VITA VIKUU SANA VILIVYOWAHI KUPIGANWA

Asante, Ndugu Orman, Bwana akubariki.

Habari za asubuhi, marafiki. Nina furaha kuwepo hapa tena asubuhi hii, na kwa namna fulani kidogo nadhani sikulitazamia, nami nina hakika isingetazamiwa na kusanyiko. Nami nilikuwa tu nina soma na (asante, Dada)—na ilionekana tu kwamba Bwana anaweka kitu kidogo moyoni mwangu kukiletea kanisa, nami nilifikiri wakati wa kukileta umewadia. Na sasa, hii—nilipowasili basi, nikiwa sijui tungekuwepo hapa Jumapili hii. Nimetangaza kwamba nina U—Ujumbe kwa ajili ya kanisa. Nami nataka, Bwana akipenda, kuleta Ujumbe huu Jumapili ijayo. Na itachukua muda mrefu sana, kwa hiyo labda hamtaondoka kabla ya saa 6.30, saa 7 labda, kama wakati huo. Umekuwa moyoni mwangu kwa muda mrefu, nami nafikiri nadaiwa na watu jibu kwa nini sikuwa na juhudi huko nje. Nami nimehubiri nikigusia juujuu, bali nina hakika, haikuja sawasawa kama ipaswavyo; kwa hiyo nafikiri, Bwana akipenda Jumapili ijayo, ninataka tu kuchukua muda wangu na kueleza tu sababu yake na kwa nini, na kuwaonyesha kimaandiko yanayoendelea. Unaona? Kuwaeleza maana yake, kwa sababu labda nitazuru nchi za ng'ambo au mahali fulani mara moja. Ninangojea sasa kuona ni wapi Yeye ataniita niende.

Siku zilizopita. . .Yapata kila usiku kwa siku tatu au mbili zilizopita, nilipata simu karibu na usiku wa manane, na ilikuwa kwa ajili ya kumwombea mwanamke fulani aliyekuwa hospitalini. Nao wakanipigia simu wakaniambia niombe (ila nasahau jina walilonipa kwamba. . .wakasema alikuwa rafiki wa Bibi James Bell, dada yetu hapa kanisani, dada mweusi, mwanamke mwaminifu, mzuri sana. Naamini jina hilo lilikuwa ni Shepherd, nililopewa), kwa hiyo nikatoka kitandani nikapiga magoti na—na kumwambia mke wangu (simu ilipolia ilimwamsha), basi nikasema, "Yatubidi tumwombee Bibi Shepherd, dada ambaye alipiga simu ambaye ni rafiki wa Bibi James Bell."

Kwa hiyo tulimwombea, tukarudi kitandani, na halafu mnamo saa 4 au saa 5 siku iliyofuata, nilipata simu tena; ilikuwa ni Billy, naye akasema haikuwa Bibi Shepherd, akasema ilikuwa Bibi Bell, mwenyewe. Si rafiki ya Bibi Bell, ilikuwa ni Bibi Bell, naye yuko hospitalini mahututi. Na nilipokimbia kwenda kule hospitalini, tayari ameaga dunia. Bwana amemwita Bibi Bell nyumbani.

Bibi Bell alikuwa mshiriki mwaminifu pamoja nasi hapa kanisani kwa miaka mingi. Mumewe, mimi na mumewe, James, tulifanya kazi pamoja na baba yangu miaka mingi iliyopita nje huko kuendesha —kuvileta vichokoo kutoka Pennsylania mpaka hapa Colgates miaka mingi iliyopita, nadhani miaka thelathini iliyopita au zaidi. Nasi tunampenda Dada Bell; alikuwa mtu mwenye heshima.

Nami nafahamu alishikwa na ugonjwa mbaya wa kibofu cha nyongo, nao hao—tabibu wake aliyejua ugonjwa ule vizuri sana alikuwa nje ya mji wakati ule, basi tabibu mpya akaja kumwangalia halafu akashauri upasuaji wa dharura, naye hakuishi. Na—na yeye alikuwa . . . nafikiri yule ninino . . . Ninavyofahamu mimi, ni kwamba tabibu wake wa sikuzote asingeagiza huo—huo upasuaji, kwa sababu alikuwa mnene, na kibofu chake cha nyongo kilikuwa kibaya, naye amekuwa na mawe, nafikiri, au kitu fulani ndani yake, na—na Bwana alikuwa amemrehemu. Alikuwa na maumivu hayo hapo awali, na Bwana aliyaangalia hayo mara nyingi, bali ikawa kwamba . . . Vema, kama tukilileta kwenye kipimo kamili tungesema hivi; Mungu amemwita Dada Bell, na hivyo ndivyo inavyopaswa kuchukuliwa. Unaona?

Na jinsi ambavyo alikosea—alilileta hilo kwangu, kwamba nilifikiri ilikuwa Bibi—Binti Shepherd; sikumjua Binti Shepherd. Binti huyo huenda akawa hapa asubuhi hii, nami huenda nikamjua kama nikimtazama. Bali ilisemwa ilikuwa Bibi Shepherd; na kama yote yalitendeka namna hiyo, kwamba kama—kama ningejua ilikuwa ah—Bibi Bell amekuwa katika hali ile, labda ningekwenda huko na kuanza kumwombea moja kwa moja; kisha, unaona, kwamba—Mungu hakutaka sisi tufanye hilo labda. Kwa hiyo tunajua ya kuwa mambo haya yote hushiriki kazi moja ndio kuwapatia mema wale wampendao Mungu. Nami nina hakika kwamba Dada Bell alimpenda Bwana wetu; alikuwa mwanamke mwema.

Sasa, yeye ni mmoja wetu. Ndani hapa hatuna mipaka yo yote ya rangi; familia ya Mungu haiweki mipaka ya rangi. Kama tu wekundu, kahawia, weusi, au manjano haijalishi —weupe, hata iwe nini tu ndugu na dada katika Kristo; na kwa hiyo tu—tunampenda, nasi tutamkosa, sisi wa maskani haya. Jinsi nitakavyozikosa hizo—hizo "amina" kubwa mno za sauti isiyo laini nyuma kule pembeni za Dada Bell, na katika kumpeleka nyumbani angezungumzia kuhusu Bwana Yesu.

Nami kama nafahamu sawa (sikujua hilo mpaka tu muda mchache uliopita), bali nafikiri mazishi yake yatakiuwa papa hapa kanisani Jumanne hii ijayo saa 7, nafikiri mimi na wewe yatubidi tushiriki rasmi katika ibada hii ya mazishi.

[Ndugu Branham anazungumza na Ndugu Neville—Mh.]

Bali katika kusanyiko, kwa kuwa tumepungua nguvu kwa mmoja asubuhi hii, katika kumheshimu Dada yetu Bell hebu tusimame tu kwa miguu yetu kwa muda kidogo tu, tukiinamisha vichwa vyetu.

Mungu wa uzima, Ambaye unatoa na kuuchukua uhai, kama Ayubu wa kale alivyosema, "Bwana hutoa na Bwana hutwaa; Jina la Bwana libarikiwe." Miaka michache iliyopita Wewe ulimtuma Dada Bell miongoni mwetu awe raia mwenzetu pamoja nasi wa Jumuia kuu ya Mungu. Nasi twakushukuru Wewe kwa kutia moyo ambako alitutia, jinsi ambavyo alipenda kuimba, na kushuhudia, na angejazwa sana na Roho mpaka angepiga kelele na kupaza sauti. Na hakuonea haya Injili ya Yesu Kristo, kwani kwake Hiyo ilikuwa nguvu ya Mungu kwa wokovu. Kuona miaka yake imehesabiwa, na saa yaja wakati sote yatupasa kujibu. Na Wewe umemwondoa kwetu asubuhi hii apate kuwa katika Uwepo Wako, kwani ni hakika kwamba tuondokapo hapa tuko katika Uwepo wa Mungu.

Ee, Mungu, tunakushukuru Wewe kwa yote. Tunaomba kwamba Wewe utambariki mumewe, rafiki yangu, James, mwanawe, binti zake, wote wale ambao. . .Tunasikia kwamba mwanawe anaruka kwa ndege kutoka Ujerumani, kutoka jeshini, kuja nyumbani kutoa heshima za mwisho anazoweza duniani, kwa mama yake aliyeaga dunia. Jinsi hapana budi moyo wa kijana yule unapigapiga asubuhi hii. Ninamwombea, Bwana. Mungu umbariki. Mbariki Jimmy, na jinsi yeye—unamwona akifanya kazi huko nje na masaa ya uchovu kupata riziki kwa ajili ya jamaa yake. Basi naomba kwamba hiyo jamaa kubwa hivi haitatenganishwa, bali gurudumu la jamaa halitavunjika katika nchi ile kule ng'ambo.

Hebu sisi, Bwana, sasa tukaze silaha zetu na ule mshipi ukazwe zaidi, na kutoka kwenda vitani sasa, kupigana huku tumepungukiwa na mtu mmoja kuliko tulivyokuwa juma lililopita, na tunaomba kwamba Wewe utatuhifadhi, na kutuimarisha, na kutusaidia tunapoendelea. Na siku moja sote na tukusanyike pamoja tena kule ng'ambo. Kwani tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa, roho ya dada yetu aliyeaga dunia na ikae katika amani.

Ningependa kusema kwamba ma—mazishi yake yatahubiriwa hapa Jumapili—au Jumanne, na tunge—kila mtu anayeweza kuyahudhuria amekaribishwa. Na nadhani Ndugu Neville hapa ana hiyo mipango na. . .Unayo. [Ndugu Branham anazungumza na Ndugu Neville—Mh.]

Sasa, leo mimi ni. . .Unaona hakuna wengi mno, kama kungeweza kuwa na kiti mahali fulani kiletwe kwa ajili ya Ndugu na Dada Slaughter nyuma kule. . .Nilipata simu yako, Dada Slaughter, na nikaenda kumwombea ninino—yule Dada Slaughter mwingine, Dada Jean Slaughter aliye na homa ya

sungura, tularemia. Yeye kweli ni mahututi, bali tunamtumaini Mungu kwamba atakuwa mzima.

Sasa, tunataka kusoma baadhi ya Maandiko, nami nataka tu kufundisha asubuhi hii, nikichukua wakati wangu, sababu tangu niliporudi kutoka Arizona, naam, koo langu lina maumivu kidogo. Na sasa, Jumapili ijayo msisahau —na nafikiri Billy tayari amekwisha peleka yale—yale matangazo na itakuwa ni ibada ndefu sana tunaamini, kwa hiyo njoni mapema na—kadiri muwezavyo. Tunataka kuanza kwenye 3.30—au ninamaanisha saa 4 na labda—kumbukeni mnamo saa 7.00 au 7.00—au labda 6.30, 7.00, kitu kama hicho, masaa matatu manne au zaidi.

Nataka kuchukua na kuchukua tu Maandiko (leteni penseli zenu na karatasi) na myaandike. Kukiweko na swali lo lote, liulize (unaona?) na labda twaweza kulielezea, kufanya tuwezalo kusaidia.

Sasa, hebu tusome baadhi ya Maandiko kwanza. Sasa, nina sehemu tatu katika Biblia ambazo ningetaka kusoma. Na ya kwanza (kama unataka kuiandika na iwapo una penseli) — nataka kurejea asubuhi hii kwenye vifungu vingi ambavyo ninge—au Maandiko mengi, hasa, ambayo ningetaka kuyarejea. La kwanza litakuwa I Petro 5:8-10, Waefeso 6:10-17, na Danieli 12:1-14.

Sasa, katika kusoma, tukichukua wakati wetu (na karibu kila mtu ameketi, kwa hiyo—wachache bado wanasimama huko nyuma na kando kando, bali tutajaribu kumaliza haraka iwezekanavyo na kuwaacha mfumukane. Kisha tutawaombea wagonjwa.

Tuna maskini bibi mdogo, anayelala hapa asubuhi ya leo, ambaye ni mahututi sana. Nasikia kwamba alikuwa mgonjwa sana jana. Na mimi—nami nilitaka tu asikize asubuhi hii kwanza kabla sijamwombea. Nami najua hali za yule bibi, naye ni mahututi; bali tunaye Baba yetu mkuu sana wa mbinguni Ambaye ameshinda kabisa maradhi yote.

Nami nina ninino ndogo (Namsihi Bibi Wood kama angeisoma, bali yeye—yeye hajisikii kufanya hivyo) makala fulani ambapo daktari wa madawa hakika alishangazwa, alipokuwa mpinzani wa kuponya Kiungu na hata hangemruhusu mtu ye yote azungumzie jambo hilo afisini mwake, na nesi wake pia. Kwa hiyo ilitokea kwamba, alipata mgonjwa ambaye alikuwa na ugonjwa wa kansa—kansa kubwa. Hakutaka kujihusisha nalo, kwa hiyo akampeleka kwenye hospitali nyingine. Hawakutaka kujihusisha na jambo hilo huko, kwa hiyo wakamrudisha. Kwa hiyo wao . . .

Loo, ilikuwa kwenye titi, na ilikuwa katika hali mbaya sana; na ngozi yote ilikwishaliwa, na ile kansa ikaingia katika titi, hata mbavuni. Nadhani mnaelewa ninalomaanisha. (Nina daktari mdogo rafiki toka Norway ameketi humu pamoja nasi

asubuhi hii.) Naye alitayarisha vyombo vyake vyote, kwa maana alisema alijua kwamba—kwamba yule bibi alimtaka amfanyie upasuaji na aondoe lile titi. Nayo ilikuwa kazi yenye damu nyingi sana, na—naye alichukua vifurushi vyake na kila kitu. Yule nesi alimtayarisha yule mama na kumleta kwenye chumba cha upasuaji, na halafu akarudi kwenda kuchukua vyombo ku—ambavyo vingetumiwa, na daktari na msaidizi wake kukata lile titi. Basi walikuwa na mataulo na kadhalika mle. Na kwa hiyo wakaanza—alipoanza kugeuka . . .

Mumewe alitaka kujua iwapo yeye angeweza kuketi pembeni mwa chumba kile aombe; alikuwa mhubiri wa utakatifu. Naye akaketi pale kando ya—mguu wa kitanda na kuomba. Bila shaka daktari hakuridhishwa vema sana na jambo hilo, unajua, na—yeye kuwepo mle ndani. Bali maadamu hataangalia, na halitamuudhi, naam, nadhani ilikuwa sawa—hange . . .?. . . hangezimia.

Kwa hiyo wakati hilo—akiwa ameketi anaomba, kukaja kupigapiga mabawa kwenye kile chumba; naye daktari anageuka aende kwenye—akiwa na vyombo vyake kuanza kuondoa lile titi; aliondoa fungu baada ya fungu na hapakuwa hata na kovu kwenye titi —hata kovu! Akasema, "Hai—ina—inahama?" Naye akaanza . . . Na yule nesi akatoa ushuhuda wake. Wote wawili walitoka na wamekuwa Wapentekoste, wamejazwa Roho Mtakatifu, wakimtumikia Bwana.

Hakuna hata kovu! Daktari Holbrook alishuhudia mwenyewe, akasema, "Dakika moja kabla ya hapo, kulikuwepo yule—yule mwanamke amelala pale, na yule nesi, huku kansa kubwa mno imetokeza yote kwenye titi lake; na dakika moja baadaye hapakuwa hata na kovu ambapo ingeondolewa." Huyo ni mmoja wa madaktari wetu hodari hapa Marekani. Alisema alisadikishwa papo hapo, na yeye—hata hivyo alikuwa ni shemasi katika kanisa. Unaona?

Unaona, watu hufikiri kanisa ni mahali tu unapokwenda tu na ni—loo, unaenda mle kujifunza kuwa mzuri au jambo kama hilo. Sivyo ilivyo, jamani. La! Mungu ni Mungu; Yeye ni mkuu vile vile leo kama Yeye alivyokuwa—alivyowahi kuwa na Yeye sikuzote atakuwa vivyo hivyo. Na Yeye ni . . . Tunampenda tu.

Sasa, tunataka kusoma sasa kutoka I Petro sura ya 5, tusome aya ya 8 na ya 10 kwanza:

> *Mwe na kiasi . . . na kukesha; kwa kuwa mshtaki wenu ibilisi, . . . simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze:*
>
> *Nanyi mpingeni huyo,* kwa uthabiti . . . *katika imani, mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani.*
>
> *Na Mungu wa neema yote, aliyewaita kuingia katika utukufu wake wa milele katika* Yesu Kristo, ninyi

mkiisha kuteswa kwa muda kidogo, yeye mwenyewe atawatengeneza, awathibitishe, awatie nguvu, na *kuwaimarisha.*

Jinsi gani Mungu asifiwe!

Sasa, katika Kitabu cha Waefeso. . .Tungependa kufungua hapa kwenye Kitabu cha Waefeso sura ya 6, na tungetaka kusoma toka aya ya 10 hadi ya 17 ambapo nimetia alama.

Hatimaye, ndugu zangu, mzidi kuwa hodari katika Bwana, na katika uweza wa nguvu zake.

Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani.

Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza la dunia—*la dunia hii, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.*

Kwa sababu hiyo twaeni binafsi *silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushinda siku ya uovu,. . . mkiisha kuyatimiza yote, kusimama.*

Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni,. . .na kuvaa dirii ya haki kifuani,

Na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani;

Zaidi ya yote mkitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu.

Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu;

Sasa, kwenye Kitabu cha Danieli ningetaka kusoma mengine zaidi. Sasa, Danieli sura ya 12; na nataka kuanza kwenye ya 1 na kusoma se—sehemu ndefu kabisa ya hii, aya kumi na nne.

Wakati huo. . .Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa. . .wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata *wakati uo huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile.*

Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine wapate uzima wa milele,. . . wengine aibu na kudharauliwa milele.

Na walio na hekima watang'aa kama mwangaza wa anga; na hao wageuzao—wageuzao *wengi kutenda haki watang'aa kama nyota milele na milele.*

Lakini wewe, Ee Danieli, yafunge—yafunge. . .kitabu, hata wakati wa mwisho: wengi wataenda mbio huko na huko, na maarifa yataongezeka.

> *Ndipo mimi, Danieli, nikatazama, na kumbe, wamesimama wengine wawili, . . . mmoja ukingoni* mwa mto upande huu, na mmoja ukingoni mwa—*mto upande wa pili.*
>
> *Na mmoja akamwuliza yule mtu aliyevikwa nguo za kitani, aliyekuwa juu ya maji ya mto, Je! itakuwa muda wa miaka mingapi hata mwisho wa mambo haya ya ajabu?*
>
> *Nami nikamsikia yule mtu aliyevikwa nguo za kitani, aliyekuwa juu ya maji ya mto, hapo alipoinua mkono wake wa kuume na mkono wake wa kushoto kuelekea mbinguni; akaapa kwa yeye aliye hai milele na milele, ya kwamba itakuwa wakati, na nyakati mbili, na nusu wakati; tena watakapokuwa wamekwisha kuvunja nguvu za hao watu watakatifu, . . . mambo hayo yote yatakapotimizwa.* (Naamini nitakoma papo hapo.)

Nataka kuchukua somo (kama lingeitwa somo) kutoka hapo kutokana na hayo, kufikia uamuzi huu wa *Vita Vikuu Sana Vilivyowahi Kupiganwa.* Hayo ndiyo ninayotaka kutumia kama somo.

Sasa, jinsi nimelipata hili kwa ajili ya somo la asubuhi hii, tumerudi sasa hivi. Mimi pamoja na baadhi ya wadhamini hapa kanisani tulikuwa huko Arizona. Nasi tulitoka kwenda kule hasa kufanya mkutano hapo Phoenix na Ndugu Sharrit kwenye maskani yake. Bali nilipoona kwamba ndu—ndugu fulani alikuwa mjini, akifanya ibada katika hema, vema basi, nilijisikia kidogo sipendelei kufanya mkutano. Niliwazia kwamba labda nitaufanya Jumapili alasiri, kusudi asiudhiwe mtu ye yote katika makanisa yao; kisha basi nikaona kwamba ana ibada ya Jumapili alasiri pia. Nami nilikuwa ki—kidogo niliona wasiwasi kuhusu kuendesha ibada, na hivyo sisi ndugu, badala ya kuendelea siku nzima (kwa vile tulikuwa tumetoka kwenda kuwinda), tulienda mjini kwenye—na tukawa tayari na tukaenda kwa yule—ibada za Ndugu Allen. (Ndugu A. A. Allen alikuwa anafanya ibada.) Kwa hiyo tulihudhuria zile ibada, naye Ndugu Allen akahubiri mahubiri motomoto. Tulikuwa na—na wakati, wakati mzuri tukimsikiliza Ndugu Allen, kusikia wa—waimbaji, na kadhalika, jinsi walivyoimba, na kupaaza sauti, na tukawa na ibada nzuri sana.

Halafu basi, tuliona njiani mwote mkono wa Bwana. Po pote tulipoenda Bwana Yesu angekutana nasi. Na kuna kitu fulani kuhusu kuondoka na ukawa peke yako, nje huko nyikani. Kuna kitu fulani kuhusu hilo kwamba kama utawahi kuwa peke yako jinsi hiyo, kuna kitu fulani kinachokuvuta. Hiyo ndiyo nafikiri moja ya sababu napenda hizo sehemu za mbali huko nje. Unaondoka kwenye nguvu za adui.

Mara nyingi kama ilivyo hapa, pepo karibu hana madhara isipokuwa apate kitu cha kutendea kazi. Ana . . . Mnakumbuka wale pepo waliotolewa katika Jeshi? Walikuwa na—wanataka kufanya madhara zaidi, kwa hiyo walitaka kwenda kuwaingia wale nguruwe. Kwa hiyo pepo yabidi wapate kitu fulani cha kutendea kazi, mtu watakayemtumia. Na hivyo ndivyo Mungu afanyavyo pia. Yeye yambidi atupate sisi; Yeye anatutegemea sisi kutenda kazi kwa sisi.

Na wengi walikuja wakati tulipokuwa safarini wakiwa na ndoto, na Bwana Yesu hakushindwa kamwe bali alitoa tafsiri sahihi na ikawa tu—ikawa sawa kabisa.

Ndipo basi Yeye alikuwa mwema kwetu akatuongoza kwenye wanyama, na kutuambia walipokuwa na, wajua, kuwa tu karibu nasi jinsi hiyo; ni la ajabu tu. Tukaketi usiku kucha kwenye moto wa kambi mbali na kila mtu kwa maili kadha wa kadha, na kuangalia ule—ule moto wa kambi wenye kusinzia kwenye mizingo ya miamba na loo, ajabu kwelikweli!

Ndugu mmoja pale ambaye alikuwa na matatizo na—na mkewe ambaye alikuwa . . . Miaka mingi iliyopita aliinua kichwa chake mkutanoni ambapo kwamba nilikuwa ninaendesha ibada, nami nilikuwa nimewaomba wainamishe vichwa vyao. Nilikuwa na pepo mchafu ambaye asingemtoka mwa—mwanamke fulani kwenye jukwaa, na hata hivyo bibi yule akakiinua tu kichwa chake bila kicho. Basi yule pepo akamtoka yule mwanamke aliyekuwa jukwaani akamwendea yeye, na hii ni kama miaka kumi na minne. Na yule bibi amekuwa taabani; kiasi kwamba, hata akaingia kichaa, mpaka anafanya mambo yasiyofaa. Kwa mfano, alimwacha mumewe akaenda akaolewa na mwanamume mwingine huku anaishi na mumewe; akadai hakujua amefanya hivyo.

Na kwa hiyo ile wao—wao walijaribu kumchunguza kwa ajili ya jambo hili—je! unasemaje wakati wewe . . . ? *Usahaulifu?* Ili . . . Jamani, sijui jina hilo. Nadhani hilo ni sawa, Daktari. Bali halikuwa hilo; ilikuwa pepo. Na yeye—na yule bibi alikuwa rafiki yangu sana, bali tangu usiku huo alinichukia makusudi. (Bila shaka unaweza kuona sababu yake.)

Bali basi wakati mumewe alipokuja nasi tukapiga magoti chumbani kuomba, ndipo Roho Mtakatifu akashuka; mambo yakaisha. Kisha Yeye akamtokea mumewe usiku ule katika ndoto. Akarudi ana ndoto; alifikiri ilikuwa ni mzaha. Akatambua ni jibu hasa la kuponywa kwa mkewe. Jinsi Roho Mtakatifu alivyoshughulika! Tukashuka kwenda Tucson na Ndugu Norman na hao wengine, na hapo Bwana akaanza kufanya kazi tena katika mambo makubwa mno, na yenye nguvu na kufunua mambo. Usiku mmoja, kilichonifikisha mimi kwenye mkataa huu hapa, nilikuwa nimesimama na Ndugu Wood na Ndugu Sothman, na tulikuwa—ilikuwa mnamo saa 4 usiku nami

nilikuwa ninaangalia juu angani, na hofu kuu ikanijilia. Basi nikasema, "Hebu tazama! Jeshi lile lote kubwa la mbinguni." Nikasema, "Kila kitu kina upatano mkamilifu."

Naye Ndugu Wood akasema, "Ukiangalia nyota ndogo mbili zinazokaribiana sana hata inafanya—zinaonekana kama nuru moja."

Nikasema, "Lakini unajua, Ndugu Wood, kulingana na sayansi, katika kundi lile la nyota saba (lile kundi dogo, lile kundi kubwa), nyota zile hazionekani ziko umbali wa inchi mbili kati yao; nazo ziko mbali zaidi moja kwa nyingine kuliko sisi tulivyo mbali nazo! Na kama zingeanza kuja huku duniani zingechukua—katika mwendo wa maili elfu kadhaa kwa saa, ingelichukua mamia na mamia ya miaka kwa hizo kufika duniani." Nami nikasema, "Katika utaratibu wote huu mkubwa, mpana mno hapa, na isitoshe, wanatuambia wanaangalia kwa darubini, wanaweza kuona muda wa miaka milioni 120 ya nuru huko mbali sana, na bado kuna miezi na nyota. Na hata hivyo Mungu aliumba kila moja yazo. Naye hukaa kati yazo."

Nami nikasema, "Mahali fulani ndani mle nilipoonyeshwa, wakati fulani katika kituo cha uchunguzi, ile zodiaki, huanza na bikira, ikaja juu kupitia wakati wa kansa, na kuendelea chini mpaka la mwisho lilikuwa ni simba, Leo yule Simba. Kuja mara ya kwanza kwa Kristo ilikuwa ni bikira; kuja mara ya pili, kwa Simba wa kabila la Yuda." Kisha nikasema, "Nimejaribu niwezavyo kuona ile zodiaki, nami siwezi kuiona; bali hata hivyo, imo mle. Wale ambao wamefundishwa wanajua kwamba ipo. Ayubu aliiona; watu walizoea kuingalia; ilikuwa ndiyo Biblia siku moja. Bali katika kusanyiko lote lile la mamilioni na mabilioni ya muda wa miaka ya nuru, Mungu huketi kati ya hizo zote, Naye anatazama chini. Paulo yuko mle ndani; mama yangu yuko mle ndani mahali fulani akitazama chini."

Na niliwaza kuhusu utaratibu wa lile jeshi la mbinguni. Hakuna mmoja wao aliye nje ya mahali pake; kila mmoja hushika majira yake kikamilifu, jeshi kubwa la Mungu. Niliwaza kuhusu askari, jinsi ambavyo kama mwezi ule ungeondoka kwenye utaratibu, dunia ingefunikwa tena na maji katika dakika chache tu. Dunia ingekuwa kama ilivyokuwa hapo Mungu alipoamua kuitumia kwa—kutuweka sisi hapa juu yake. Ilikuwa ukiwa, tena tupu, na giza, na maji yalikuwa yametapakaa juu ya uso wa nchi. Na kama mwezi ule utawahi kusogea, ungefanya jambo lile lile tena. Mwezi unapotikisika kidogo ukisogea mbali na dunia husababisha maji kujaa baharini; unaposhuka, kunafuata kupwa baharini. Ni jeshi kuu la Mungu.

Na nilipofikiri kuhusu ile—hilo likiwa jeshi kuu la Mungu hapo. . .Naam, tulienda kulala, na basi nikaanza kuwazia kwamba hata moja ya hizo haiondoki mahali pake; zote ziko

mahali pao. Na kama kuna msogeo mahali po pote kati yao, ni kwa sababu fulani na itakuwa na matokeo fulani katika dunia hii. Nasi tumeona matokeo yake sasa, kutokana na baadhi yao kusogea kwenye sehemu zao zingine. Husababisha mambo; hubadili kila kitu.

Nami nikawaza basi, kama hilo jeshi kubwa kama hilo la mbinguni linapaswa kushikilia mahali pake kufanya kila kitu kiwe katika utaratibu, je! vipi kuhusu mchafuko wa jeshi la duniani? Jinsi ambavyo wakati mmoja anatoka kwenye utaratibu, jinsi inavyovuruga kila kitu. Mpango wote wa Mungu unavurugwa wakati mtu mmoja anapotoka kwenye utaratibu. Yatupasa kujitahidi sikuzote kudumisha utararibu wa Roho.

Nami ningemwomba Mungu asubuhi hii, kwamba tungelifikisha hili kwenye ibada halisi ya kuponya, kwamba tungeweza kushikilia sehemu hii—kundi ambalo tumekusanyika chini ya dari asubuhi hii katika upatano sana hata Roho Mtakatifu angemweka kila mshirika wa ule mwili aliye hapa asubuhi hii katika upatano sana, hata kungekuwa na kuponya kunakobubujika kwenyewe kwa nafsi na miili. Kama tu tungeshikilia mahali petu.

Sasa, kama nilivyosema mwanzoni, bibi huyu aliyekuwa na kansa ambayo Daktari Holbrook angechukua—angeiondoa . . . Sasa, yule Mungu ambaye alisababisha ile sauti ya kupigapiga mbawa isikike katika ile hospitali na kuondoa kansa ile bila hata ya kuacha kovu, hamjui kwamba Mungu yuyo huyo yupo hapa? Na jambo pekee ambalo Yeye anangojea ni kwa je—jeshi Lake kushika mahali pake, kama nyota—kushika mahali pake.

Sasa je, mnajua tumekuwa na vita baada ya vita na matetesi ya vita, na kama dunia ikidumu zaidi tutakuwa na vita vingi zaidi. Lakini mnatambua kwamba hasa kuna mamlaka mbili tu katika ulimwengu wote? Katika ugomvi wetu wote baina ya mataifa, na ugomvi kati ya mmoja na mwingine na kila kitu, yote inajumulika katika mamlaka mbili. Kuna mamlaka mbili tu na kuna falme mbili peke yake —mamlaka mbili na falme mbili. Mengine yote ya hayo mambo madogomadogo yanahusikana na mojawapo ya mamlaka hizo. Na mamlaka hizo ni mamlaka ya Mungu na mamlaka ya Shetani. Hilo ndilo ambalo ile—kila vita, kila mchafuko, kila kitu kinachokuja, aidha kinaongozwa na uweza wa Mungu ama nguvu za Shetani, sababu hizo ndizo mamlaka mbili zilizopo. Na hiyo ni mamlaka ya uzima na mamlaka ya mauti. Sasa, hayo ndiyo mamlaka mawili pekee.

Na Shetani anaweza tu . . . Nguvu yake aliyo nayo ni nguvu za Mungu zilizopotoshwa. Si nguvu halisi: ni upotovu wa nguvu za Mungu, kila kitu alicho nacho Shetani. Kifo ni upotovu tu wa uhai; uwongo ni ukweli tu ukielezwa vibaya. Mnaona? Uzinzi ni te—tendo lililotumiwa vibaya, tendo la haki likitumiwa

vibaya. Mnaona? Kila alicho nacho Shetani ni kitu ambacho kilipotoshwa, bali ni nguvu.

Nasi tupo leo tunaketi hapa, na moja au nyingine ya mamlaka hizo itatutawala sisi; kwa hiyo hebu na tumtoe yule mwovu. Na tuchukue mahali petu kama nyota za mbinguni.

Kama vile isemavyo Biblia, *"Nyota zipoteazo* (kwenye kitabu cha Yuda), wakitoa aibu yao wenyewe kama povu." Nasi hatutaki kuwa nyota *zipoteazo*: *kushangaa* kama hili ni sawa, *kushangaa* kama lile ni sawa, *kushangaa* kama litatukia, *kushangaa* kama—jinsi ingeweza kuwa. *Usishangae,* kaa kama nyota zile za mbinguni kama askari halisi kwenye wajibu wake! Simama hapo ukiamini! Uzima na mauti . . .

Naam, jeshi—wakati hasa jeshi—taifa linapojitayarisha kwenda vitani dhidi ya taifa jingine, linapaswa kwanza likae chini na kupima kilicho sahihi na kisicho sahihi, na iwapo wanaweza kupigana dhidi ya taifa jingine au la. Yesu alifundisha hilo. Na kama watu wangefanya hivyo, kama mataifa yangekuwa—yangeketi chini na kutulia na kufikiria mambo hayo, pande zote mbili, tusingekuwa na vita tena.

Sasa, tunaona kama mtu hafanyi hayo, kama wakuu wa jeshi wa taifa hawatakaa chini kwanza na kupima kuona kwamba wako sahihi, na nia na makusudi yao ni sawa, na kama wana nguvu za kutosha na uwezo wa kushinda jeshi jingine; basi hakika watashindwa.

Hapo ndipo ambapo Jenerali Custer alipofanya kosa lake baya sana. Jenerali Custer, kama ninavyofahamu, alipewa amri na serikali asiende kwenye nchi ya Sioux, kwa sababu ulikuwa wakati wa dini kwao. Ulikuwa wakati wa kuabudu; walikuwa wanaadhimisha sikukuu. Bali Custer akalewa, naye alifikiri kwamba angelilitenda tu kwa vyo vyote. Angelivuka, kama ni amri au siyo amri. Na ndipo kwa kweli waliwapiga risasi watu wasio na hatia—wakawatupia risasi. Nafikiri waliwapiga baadhi yao. Ilikuwa ni maskauti waliotoka kutafuta chakula kuwalisha wao—watu wao wakiwa katika ibada. Naye Custer, alipokuwa anavuka aliwaona akafikiri walikuwa wanawawinda, na kwa hiyo waliwatupia risasi hawa maskauti. Na hawa maskauti walitoroka wakarudi. Walifanya nini? Wakatwaa silaha, hawa hapa wanakuja, na huo ukawa ndio mwisho wa Jenerali Custer—kwa sababu hakuketi chini apate kufikiri kwanza.

Haikumpasa kwenda kule! Hakuwa na haki ya kuwepo kule! Alikuwa amewasukumia Wahindi kote kote toka Pwani ya Mashariki kufikia upande wa magharibi kwa vyo vyote. Nao walifanya mapatano, bali yeye alivunja yale mapatano. Naye alipovunja yale mapatano, basi akapoteza vita.

Na kwa hivyo, jeshi, kwanza katika kuwa tayari kwa vita, kwanza yapasa kuwe na ku—kuchagua baadhi ya askari. Yawapasa wavalie kwa ajili ya mapigano; yawapasa

wafundishwe kwa ajili ya mapigano. Nami naamini kwamba vita vikuu sana vilivyowahi kupiganwa sasa viko tayari kuanza. Nami ninaamini kwamba Mungu amekuwa akichagua askari Wake; naamini Yeye amekuwa akiwavalisha, akiwapa mazoezi. Na mstari wa mbele wa vita sasa umeisha pangwa, tayari kuanza.

Hivi vita vikuu vya kwanza ambavyo viliwahi kupiganwa vilianzia Mbinguni wakati Mikaeli na Malaika zake walipopigana dhidi ya Lusifa na malaika zake. Vilianza kwanza—vita vya kwanza vilikuwa Mbinguni, kwa hiyo dhambi haikuanzia duniani, ilianzia Mbinguni. Ndiposa ikatupwa chini toka Mbinguni, ikatupwa toka Mbinguni hadi duniani na kuanguka juu ya wanadamu. Kisha vita toka kwa Malaika vikawa vita vya wanadamu. Naye Shetani akaja kuharibu uumbaji wa Mungu. Kile Mungu alijiumbia, alikuwa (Shetani), amekuja kukiharibu. Hilo ndilo lililokuwa kusudi lake, ni kuangamiza. Basi vita vikaanza hapa duniani na kuanza ndani yetu, na vimewaka moto tangu wakati huo.

Naam, kabla ya vita vyo vyote kupangwa, yabidi kwanza wachague mahali pa kukabiliana au mahali ambapo vita vitapiganiwa, mahali palipochaguliwa. Katika Vita Vikuu vya Kwanza vilipangwa vizuri sana katika ardhi isiyo ya mtu na mahali ambapo wangepigania, na yabidi pawepo na mahali palipochaguliwa.

Kama wakati Israeli walipoenda vitani kupigana na Wafilisti, kulikuwa na kilima kila upande ambapo walikusanyika. Na hapo ndipo Goliathi alipotokea na akayaalika majeshi ya Israeli. Hapo ndipo Daudi alipokabiliana naye, kule bondeni, alipovuka kijito kidogo ambacho kilitiririka katikati ya vilima viwili, akaokota mawe. Inabidi pawepo mahali palipochaguliwa.

Na katika hili, kuna ma—mahali palipokubalika na pande zote, "ardhi isiyo ya mtu," nao wanapigana mahali hapa. Hawapigani vita moja hapa, na moja chini hapa, na moja papa hapa; kuna uwanja wa mapambano ambapo wao hukutana na kujaribu nguvu zao, ambapo kila jeshi hujaribu nguvu zake dhidi ya lile jeshi jingine— mahali palipokubalika na pande zote pa kukabiliana.

Sasa, usipate—usikose hili! Wakati vita hivi vikuu vilipoanza duniani, ilibidi pawepo mahali pa kukabiliana palipokubalika; ilibidi pawepo mahali palipochaguliwa pa kuanzia vita, na kwa vita kuwaka moto; na mahali vinapopiganwa vita palianzia katika akili ya binadamu. Hapo ndipo vita huanza. Akili ya binadamu ilichaguliwa kuwa uwanja wa vita, ambapo vilipaswa kuanzia; na hiyo ni, kwa sababu kwamba maamuzi hufanywa kwenye akili, kichwani.

Sasa, hawakuvianzisha kamwe katika madhehebu fulani; hawakuvianzisha katika jambo fulani la kimitambo; uwanja wa mapambano haukuanza hapo kamwe; kwa hiyo, madhehebu hayo hayawezi kamwe, hayawezi kamwe kufanya kazi ya Mungu, kwa sababu mahali pa mapambano, ambapo inakubidi kukabiliana na adui wako, ni katika akili. Yakubidi kufanya uchaguzi wako. Vitakukabili.

Nataka msichana huyu mdogo hapa ambaye ni mgonjwa sana ahakikishe kwamba anasikiliza hili sasa kwa makini sana.

Maamuzi hufanyika akilini, kichwani. Hapo ndipo Shetani anakabiliana nawe. Na maamuzi hutolewa, kwa sababu Mungu alimfanya mtu jinsi hiyo. Sasa, nime. . . Kama ulikuwa ukiangalia kwenye muhtasari wangu hapa, ramani ndogo iliyochorwa. Nilikuwa nayo hapa si muda mrefu uliopita juu ya—ilitumiwa ubaoni.

Binadamu ameumbwa tu kama punje ya ngano. Ni mbegu, na binadamu ni mbegu. Kimwili wewe u mbegu ya baba yako na mama yako, na uhai hutoka kwa baba, nyama ya mwili hutoka kwa mama. Kwa hiyo hivyo viwili pamoja, yai na da—damu vinaungana, na katika chembe ya damu kuna uhai, na mle ndani inaanza kukua kumfanyiza m—mtoto.

Sasa, mbegu yo yote ina ganda upande wa nje; upande wa ndani ni nyama, na ndani ya nyama ni chembe ya uhai. Naam, hivyo ndivyo tulivyofanywa. Tu mwili, nafsi na roho. Sehemu ya nje ya mwili, ganda, ndani ya huo (dhamira na kadhalika) ni nafsi, na ndani ya nafsi ni roho. Na roho hutawala vyote vingine.

Sasa, kama utaketi chini utakapofika nyumbani na kuchora duara tatu ndogo, utaona kwamba mwili wa nje una hisi tano ambazo huwasiliana kwazo, na hizo ni kuona, kuonja, kuhisi, kunusa, kusikia; hizo ndizo hisi tano zinazoongoza mwili wa binadamu. Ndani ya mwili ni nafsi, na hiyo nafsi inaongozwa na mawazo, dhamira, kumbukumbu, hoja, na upendo; hicho ndicho kitu ambacho huongoza nafsi! Bali roho ina hisi moja—roho. Loo, hebu tuipate! Roho ina hisi moja, na hisi hiyo aidha inaongozwa, na imani au shaka! Hilo ni kweli hasa. Na kuna njia moja pekee ya kuifikia, nayo ni hiari. Unaweza kukubali shaka au unaweza kukubali imani, mojawapo unayotaka kufanya kazi nayo.

Kwa hiyo, Shetani alianzia sehemu hiyo muhimu kusababisha roho ya binadamu kushuku Neno la Mungu. Mungu alianzia sehemu hiyo muhimu kuweka Neno Lake katika roho ile. Basi, ndivyo inavyotendeka.

Kama kanisa hili sasa hivi lingeweza kuwekwa pamoja na kuunganishwa pamoja kwa kitu kama hicho, ili kwamba kila mtu awe katika moyo mmoja, bila ya shaka hata kidogo po pote, pasingekuwa na mtu mnyonge miongoni mwetu katika dakika zingine tano; kusingekuwa na mtu ye yote hapa anayehitaji Roho

Mtakatifu, ila ambaye angempokea Huyo. Kama mngeweza tu kutengeneza hilo jambo fulani!

Sasa, hapo ndipo vita huanza—mumo humo katika akili yako, kama wewe ukitaka . . . Sasa kumbuka, si Sayansi ya Kikristo sasa, bongo juu ya maumbile ya asili; hilo halina . . . Akili hupokea Uzima ambao ni Neno La Mungu, na hapo huleta Uzima. Wazo lako pekee halilifanyi, bali Neno la Mungu likiletwa katika mkondo wa wazo lako. Unaona? Siyo wazo, kama Sayansi ya Kikristo inavyolifanya, akili juu ya maumbile ya asili. La! Si hilo. Bali akili yako hulipokea na kulishika. Akili yako huongozwa na nini? Roho yako; na roho yako hulinasa Neno la Mungu, na hicho ndicho kitu ambacho kina Uzima ndani yake. Linaleta Uzima ndani yako.

Loo ndugu, hilo linapotendeka, wakati Uzima hushuka chini kwenye mkondo ule kuingia ndani yako, Neno la Mungu linadhihirishwa ndani yako. "Ninyi mkikaa ndani Yangu na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, basi ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa."

Basi hilo linatenda nini? Toka katikati ya moyo, ambayo ni nafsi, tokea hapo huenda, kulisha kila mkondo. Tatizo ni kwamba tunasimama hapa tukiwa na mashaka sana tukijaribu kupokea lililoko pale nje. Yakubidi uache hilo na uje kwenye mkondo ule na Neno la kweli la Mungu, na ndipo linatoka, lenyewe, bila ya kushurutishwa. Ni kile kilicho ndani. Hicho ndicho kitu cha maana, ni kile cha ndani. Shetani huanza kutukabili upande wa ndani.

Naam, unasema, "Siibi; sinywi; sitendi *mambo haya*." Hayo hayahusiani na jambo hilo (unaona?), ni mle ndani. Haidhuru u mzuri jinsi gani, jinsi ulivyo mwadilifu, jinsi ulivyo wa kweli, mambo hayo yanaheshimika, bali Yesu alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili . . . " Unaona? Yabidi kitu kitendeke mle ndani. La sivyo, hayo ni mambo ya kuigiza kwani chini ndani ya moyo wako unatamani kutenda jambo hilo kwa vyo vyote.

Hakiwezi kuwa cha kuigiza, chapaswa kiwe halisi. Na kuna njia—njia moja tu ambayo hicho chaweza kushukia, na hiyo ni kwa hiari ya mtu, huja katika nafsi kwa mawazo yako. "Maana mtu aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo. Kama ukivambia mlima huu, 'Ng'oka' na usitie shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba ulilosema litatukia; litakuwa lako." Unafahamu? Basi. Unaona? Huo ndio uwanja wa vita.

Kama ungeanza tu hilo kwanza. Tunatamani sana kuona mambo yakitendeka; tunatamani sana kumtendea Mungu kazi. Maskini bibi huyu anamtamani sana—bila shaka anatamani kuishi; anataka awe mzima. Wengine wapo hapa, wanataka kuwa wazima. Na tunaposikia kuhusu jambo hilo, kama yule daktari, kufufuliwa kwa wafu, mambo makuu ya uweza ambayo Mungu wetu ametenda, basi tunatamani mno. Na jambo ni

kwamba, tunajaribu kwa hisi hizi kushika jambo fulani hapa, kama dhamiri.

Watu wengi sana mara nyingi wamekosa kuelewa vema Neno, nami nimeeleweka vibaya kwa jambo hili, kwa kutoa mwito wa madhabahuni. Nilisema sishikilii sana miito ya madhabahuni; simaanishi kwamba hupaswi kutoa mwito wa madhabahuni, bali mtu fulani anamshika mtu mkono akasema, "Loo, Ndugu Yohana, unajua nini? Mimi na wewe tumekuwa majirani wakati wote huu; njoo huku madhabahuni; piga magoti."

Anafanya nini? Laiti ningelikuwa na ubao hapa, ningeweza kukuonyesha analofanya. Anajaribu kutenda kazi kwa nafsi yake katika upendo. Hilo halifai kitu! Hiyo siyo ile njia! Hakika siyo. Pengine anashughulika katika nini? Kumbukumbu, kupitia hisi ya nafsi yake. "Loo, Ndugu Yohana, ulikuwa na mama mzuri sana; alikufa muda mrefu uliopita"—kumbukumbu. Unaona? Huwezi kufanya hivyo, inabidi lishuke kwa njia ya hiari ya mtu. Wewe, mwenyewe, ruhusu Neno la Mungu. . . Huji eti kwa sababu mama yako alikuwa mwanamke mwema, huji kwa sababu wewe u jirani mwema; unakuja kwa sababu Mungu anakuita uje, nawe unamkubali Yeye juu ya msingi wa Neno Lake. Hilo Neno ndilo linalomaanisha kila kitu.

Hilo Neno, kama unaweza kuondoa kila kitu njiani—dhamiri yote, hisi zote —na kuruhusu Neno liingie ndani, Neno hilo litazaa vivyo hivyo hasa.

Hapa, unaona limefunikwa na nini? Unasema, "Vema, sasa, a—haa . . . " Unasema, "Vema, hizi dhamiri, na hisi, na kadhalika hazihusiani nalo, Ndugu Branham?" Hakika zinahusika! Bali iwapo utaliruhusu Neno liingie na kulifunika na dhamiri, basi haliwezi kukua, litakuwa neno lemavu. Je! uliwahi kuona punje nzuri ya mahindi iliyopandwa ardhini na kuachia kijiti kiiangukie, itakua imejipinda. Mtu ye yote, cho chote ambacho hukua kitafanya hivyo, kwa sababu kitu fulani kimekizuia.

Naam, hiyo ndiyo shida ya imani yetu ya Kipentekoste leo. Tumeachilia mambo mengi mno yaizuie, imani ambayo tumefundishwa, Roho Mtakatifu ambaye amekuwa akiishi ndani yetu. Tumeachilia mambo mengi mno—tukimwangalia mtu mwingine, na ibilisi sikuzote anajaribu kukuonyesha kushindwa kwa mtu, lakini anajaribu kukuondoa kwenye ushuhuda halisi ambao ni wa kweli. Atakuonyesha mnafiki wakati mwingine, ambaye ametoka kwenda kuigiza jambo fulani. Hakufanikiwa, kwa sababu alikuwa anaigiza. Bali kama asili yake ni Neno la kweli la Mungu, "Mbingu na nchi zitapita bali Neno Langu haliwezi kupita." Lazima lidumu. Unaelewa, Dada?

Yabidi lipokewe akilini; kisha linaaminiwa kwa moyo; ndipo Neno la Mungu linakuwa jambo halisi; ndiposa kila hisi za nafsi na mwili inasuguliwa sana kwa Roho Mtakatifu. Ndipo

wewe ni hisi ya Mungu; wewe ni dhamiri ya Mungu; kila kitu kinachomcha Mungu kinatiririka kupitia kwako. Hakuna shaka po pote. Hakuna cho chote kiwezacho kujiinua. Hakuna cho chote kinachoweza kuja kwenye kumbukumbu na kusema, "Vema, ninakumbuka Binti Jones alijaribu kumtumaini Mungu. Bi *fulani,* Bi. Doe alijaribu kumtumaini Mungu kwa kuponywa wakati mmoja, akashindwa." Unaona? Bali kama mkondo ule umefagiwa, na kutakaswa, na kujazwa ndani kwa Roho Mtakatifu, hilo hata halikumbukwi. Mambo ya Bi Jones na aliyofanya si hoja, ni wewe pamoja na Mungu, na si mtu mwingine bali ninyi wawili. Hivyo ndivyo ilivyo; hivyo hapo vita vyako.

Muue papo hapo mwanzoni; mkomeshe kabisa anapokuja! Si eti unaweza kuendeleza vita muda gani, ni kuvikomesha sasa hivi. Kama utakuja, na utashikilia hayo makumbukumbu, na dhamiri, na kila kitu kufikiria kuhusu, "Naam, huenda nikashindwa. Huenda ikawa si sahihi." Usifanye hilo kamwe! Tupilia kando kila kitu na ufungue ule mkondo useme, "Mungu, Neno Lako ni Kweli Milele, Nalo ni kwa ajili yangu. Kama kanisa lote likishindwa, kama ulimwengu wote ukishindwa, bali mimi siwezi kushindwa, kwa sababu ninachukua Neno Lako."

Hivyo hapo vita; jambo ndilo hilo. Vipi Mungu Mwenyezi aondoe kansa katika titi la mwanamke bila ya kovu na kumwacha mtoto alale na afe? La, bwana!

Msichana mdogo alikuja hapa si muda mrefu uliopita kutoka shule ya sekondari. Mama yake akanipigia simu, akasema, "Ndugu Branham, msichana wangu ana ugonjwa wa kuvimba wengu na ini." (Hiyo ni kansa ambayo hufanya marugurugu.) Nao madaktari wakachukua kipande kilichotumbuka toka kwenye koo lake, wakakipeleka, na ilikuwa ni ugonjwa wa kuvimba wengu na ini kweli.

Kwa hiyo akasema, "Kingine kikitumbuka huenda kikatumbuka katika moyo wake; jambo hilo likitukia, ataaga dunia." Akasema, "Hana—namna vinavyotumbuka, ataishi tuseme yapata miezi mitatu."

Yule mama akasema, "Nifanye nini, nimrudishe shuleni?"

Kasema, "Mwache aende kwa sababu labda atakufa ghafla." Na akasema, "Mwache tu aende aishi maisha ya kawaida tu awezavyo. Usimwambie kitu kuhusu hilo jambo."

Kwa hiyo yule bibi akaniambia, "Nifanye nini?"

Nikasema, "Mlete umuweke kwenye mstari wa maombi." Kisha nikasema, "Njoo pamoja naye!" (Nikahisi jambo dogo geni.)

Na wakati yule msichana alipokuja asubuhi ile na midomo ya samawati kutokana na kujipodoa, na shule hiyo inayo mambo hayo, na—na maskini msichana huyo akaja kule (sikujua yeye

ni nani, ilikuwa wanipigie simu.) Nikamshika mkono wake; nikasema, "Habari za asubuhi, Dada." Huyo hapo; ilikuwa ni yeye. Mnamo muda kidogo nalitazama kule chini kwa mamaye na kuona wote wawili bila Mungu, bila Kristo. Nikasema, "Mnategemeaje kuponywa kwenye misingi hii? Mtampokea Yesu Kristo kama Mwokozi wenu binafsi?" Nikasema, "Mtakuja kwenye dimbwi hili hapa mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu?"

Wakasema, "Tutafanya hivyo!" Loo, mnajua kilichotukia!

Huenda huyo mwanamke ameketi hapa asubuhi hii. Wengi wenu mnajua kisa hicho. Ndugu Mike Egan, mmoja wa wadhamini hapa, alifuatilia kisa hicho; hiyo imekuwa kama miaka minne, mitano iliyopita. Huyo msichana mdogo alirudishwa kwa daktari; hakuna hata alama ya ugonjwa wa kuvimba wengu na ini ulioonekana ndani yake.

Shida ilikuwa ni nini? Ilikubidi kufungua ule mkondo kwanza! Inakubidi umweke yule Askari, Roho Mtakatifu, kwenye mstari wa mbele wa mapigano inahitaji Neno la Mungu; Yeye ni Neno, Naye anasimama pale; na hakuna cho chote kinachoweza kumzuia basi. Hakuna cho chote—kila moja ya hiyo mikondo mingine imefagiliwa.

Ni kama tu vile chombo kikuukuu cha kuchemshia maji chenye bomba lililozibika; unaweka moto, nalo litalipua chombo chako. Hiyo ndiyo shida ya Wakristo wengi sana waliolipuliwa ni kwa sababu hawaisafishi mikondo; hawashuki wakaingia mle ndani. Inakubidi kuisafisha—dhamiri, kumbukumbu, fikara—kuweka kando kila kitu na kuja kutoka ndani hadi nje pamoja na Neno la Mungu lisiloghoshiwa, kwamba Hilo ni Ukweli. Haidhuru kama elfu kumi walikufa upande huu leo wakitumaini, kumi elfu walikufa upande ule kesho wakitumaini, hilo halihusiani na mimi. Ni mimi binafsi, mimi ndiye ninayetumaini; mimi ndiye ninayeliamini!

Nasi tunaona nyuma huko, kama tukitaka kufungua mikondo yetu basi, kama tunaweza na kuona, tunaona huyu na yule, na huyu na yule, maelfu wao wakishuhudia, lakini ibilisi atajaribu kurudi tena. Unaona, kama anaweza kuingia tu mle ndani kabisa, ameliangamiza jeshi lako papo hapo. Iwapo una hisi zako—kuona, kuonja, kuhisi, kunusa, na kusikia, hizo ni sawa, bali usizitumaini isipokuwa zinapatana na Neno. Ziko sawa, bali kama hazipatani na Neno, usizisikilize.

Sasa, mawazo, dhamiri, kumbukumbu, fikara, na upendo, ziko sawa, kama zikiambatana na Neno. Bali iwapo upendo wako haupatani na Neno, ukatae; utalipua bomba upesi sana. Unaona? Kama hoja yako haiambatani na Neno iache! Hilo ni kweli. Ule mtambo . . . Kama kumbukumbu lako, kama mawazo yako, kama dhamiri zako, cho chote kile hakiambatani na hilo, kile kilicho ndani, kiondoe!

Una nini basi? Una mfumo wa jua. Haleluya! Mungu aliziweka nyota katika utaratibu kisha akasema, “Ning’inieni hapo hata nitakapowaita.” Zinakaa mle. Hakuna kitakachoziondosha. Wakati Mungu anapoweza kumpata mtu mikononi Mwake, hata yeye aweze kusafishwa hisi, dhamiri na kila kitu, mpaka inasimama na Mungu nyuma yake katika Roho; hakuna pepo duniani awezaye kuingiza shaka mle ndani! Hiyo ni kweli.

Kama akija na aseme, “Ungali unaumwa,” dhamiri yako hata imekufa kwa hilo. Bomba ni safi sana hata linapaza sauti, “Haleluya.” Tundu hilo linapiga filimbi; “Mungu atukuzwe!” Linatoa sauti, kwa hakika ni safi na dhahiri sana kwa Neno la Mungu kutenda kazi kwake, uweza wa Mungu. Unaona? Hilo ndilo jambo muhimu; hapo ndipo penye uwanja wako wa vita. Uwanja wako wa vita uko nyuma hapa mwanzoni, nyuma hapa kwenye nafsi, nyuma kwenye akili yako inayofunguka. A—akili ndiyo lango la kuingilia kwenye nafsi—namaanisha lango la kuingilia kwenye roho. Akili yako hufunguka na kumkubali Roho au inamkataa Roho.

Waweza uwe na dhamiri ndogondogo, na hisia ndogondogo, na mishtuko midogomidogo, mambo yote haya; hayahusiani kwa lo lote na hilo. Hiyo ni mishtuko midogomidogo tu na kadhalika. Bali ijapo kwenye jambo halisi, akili yako hufunguka. Akili yako aidha inalikubali au inalikataa! Ndivyo ilivyo, marafiki. Mungu, jalia asiweko mtu ye yote kati yao atakayelikosa! Unaona? Ni akili yako ambayo hufungua mlango (au kufunga mlango) na kusikiliza dhamiri zako, kusikiliza kumbukumbu lako, kusikiliza upendo wako. Bali wakati akili yako inapojifungia yenyewe kwa mambo haya na kumruhusu Mungu, Roho wa Neno Lake, aingie, Huyo hutimua kila upuzi nje! Kila shaka ametoweka; kila hofu imetoweka; kila mshtuko wa shaka umetoweka; kila hisi imetoweka! Hakuna kitu kinachosimama hapo ila Neno la Mungu, na Shetani hawezi kupigana na Hilo! La, bwana! Hawezi kupigana Nalo. Naam, tunajua huo ni Ukweli.

Vita hivi vimepiganwa tangu siku ya bustani ya Edeni, vita katika akili ya binadamu. Shetani aliianzisha. Alifanya nini alipokutana na Hawa? Hakukana Neno la Mungu, bali alilipaka chokaa. Aliziba baadhi ya mikondo midogo hapa mahali fulani. Alisema, “Lakini hakika Mungu . . . (Mwanzo 3:1. Unaona?) Hakika Mungu . . . Mambo yote haya ambayo Yeye—Yeye—Yeye aliahidi . . . ” Alijua Neno lilikuwa kweli, bali alijua hangeweza kuja tu moja kwa moja na kulilipua Hilo kwa kishindo jinsi hiyo, bali yeye—yeye—alilitia sukari.

Kama mama alivyozoea kutunywesha dawa, na—naye angejaribu kuweka maji ya machungwa katika mafuta ya mbarika. Jamani, afadhali kunywa mafuta ya mbarika bila ya maji ya machungwa. Kitu cho chote ambacho ni cha kinafiki!

Unaona? Yeye—tulizoea kulazimika kuamka wakati wa usiku, naye angetupa mafuta ya samaki kwa ugonjwa wa kusongwa na koo. Basi aliweka mafuta ya samaki na kuyatia sukari. Unaona? Kiunafiki kwa namna fulani, lakini yangeviwasha tu vivimbe vya kooni mwako yakishuka baada ya sukari kwisha.

Vema, hivyo ndivyo ilivyo, marafiki. Shetani hujaribu ku—kuwa mnafiki kuhusu hilo. Hujaribu kukuonyesha kitu ambacho ni bora zaidi, njia rahisi zaidi, mpango ulio wa busara zaidi. Bali hakuna mpango wa busara zaidi kuliko ule ambao Mungu aliuweka hapo mwanzo—Neno Lake! Shikilia hilo Neno; lishike Hilo kabisa! Liache Hilo likushike kabisa! Dumu hapo Nalo! Hivyo ndi—hivyo ndivyo ilivyo.

Vita viliwaka moto wakati Hawa alipofungua akili yake kusikiliza hoja zake. Hilo ndilo bomba ililoingilia; huo ndio ule—ule mkondo ilimotiririkia—hoja zake. Yeye katika nafsi yake, alihoji. Macho yake, kwa macho alimwona nyoka. Yeye alikuwa mrembo, mzuri wa uso, mzuri sana kuliko mumewe. Alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwituni. Naye alikuwa labda mwanamume mzuri zaidi kuliko mumewe; alionekana kama mnyama mkubwa wa kiume aliyesimama pale. Jinsi alivyokuwa mkubwa, naye alikuwa anajaribu kumwambia mwanamke jinsi kilivyokuwa kitu kizuri. Na jambo la kwanza mwanamke alilotenda, alifungua bongo lake. Naye alipolifungua, hoja za kibinadamu zililikamata. "Mbona, hivi jambo hilo lisingalikuwa jambo la kusisimua!"

Hilo ndilo jambo atendalo kwa mwanamke leo. Mwanamke fulani mwenye mwanamume mdogo anayependeza anapata jitu kubwa, pandikizi la mwanaume; mwanamume huyu atajaribu kuanzisha mahojiano. Kumbuka, huyo ni Shetani; huyo ni ibilisi! Au vinginevyo, mwanamume kwa mwanamke, mwanamke kwa mwanamume, njia yo yote. Anafanya nini? Anatenda kazi katika ule ustadi wa kuhojiana, ile dhamiri au jambo fulani huanza kuingia ndani, bali lipe Neno la Mungu nafasi ya kwanza.

Mtu hata hawezi kuja . . . hawezi kutenda dhambi. Haleluya! Hili hapa, hili linakuja moja kwa moja. Mtu hawezi kutenda dhambi mpaka kwanza aweke kando Neno la Mungu! Hawezi hata kutenda dhambi (yaani kutokuamini) mpaka kwanza aondoshe Neno la Mungu, Uwepo wa Mungu; hawezi kutenda dhambi.

Hawa hakuweza kutenda dhambi, mpaka alipoweka kando Neno la Mungu, akafungulia mkondo wake wa mahojiano katika nafsi yake naye akaanza kutoa hoja. "Mbona hakika, mume wangu hajawahi kuniambia mambo haya, bali ninaamini kwamba wewe . . . Yeye aliniambia hainipasi kutenda jambo hili, bali unajua, wewe unalifanya liwe halisi sana; ni dhahiri mno.

Ninaamini lingekuwa jambo zuri sana, kwa sababu unalifanya dhahiri mno kwangu."

Unaona? Hivyo hapo vita vya kwanza. Na kwa vita vile amesababisha kila vita vingine na kumwagika damu kwo kwote kulikowahi kuja kulisababishwa pale pale katika Edeni. Hakuamini Neno la Mungu.

Na kama yodi moja ndogo ya Neno la Mungu haikuaminiwa, ilisababisha taabu zote hizi, tutarudije, huku hatuliamini Neno? Huwezi ukalitenda. Yakubidi ufungie nje mambo haya mengine yote, dhamiri, kumbukumbu na tuseme—hoja na haya mambo mengine yote, "tukitupilia mbali mahojiano." Hatuhoji jambo hilo kamwe, la hasha. Tunalikubali tu Neno juu ya msingi, "Mungu alisema hivyo"; na linafanya kijito kati yako na Mungu. Kila mkondo unafunguka kati yako wewe na Mungu basi. Hivyo hapo vita, mstari wa mbele hasa.

Hebu na tusitumie bunduki aina ya .22. Hebu tuchukue bo—bomu la atomiki. Hebu na tuitende kazi sawasawa. Hebu tuchukue bomu la atomiki la Mungu. "Ni nini, Ndugu Branham?" I-m-a-n-i katika Neno Lake! Hilo ndilo bomu la atomiki la Mungu, Nalo hutimua maradhi na pepo kulia na kushoto. Hilo—Hilo huyaangamiza, huyabagua. Loo, Hilo hu—hu—huyaharibu tu; Nalo huvunjavunja kila kitu ambacho hakimchi Mungu. Wakati bomu hilo la imani linapoanguka mle ndani na Neno la Mungu nyuma yake, hutimua kila pepo, kila maradhi, kila ugonjwa.

Unasema, "Hivi hilo ni sawa, Ndugu Branham? Basi, kwa nini linatenda kwa watu fulani na sio kwa wengine?" Ni kwa sababu ya ule mkondo. Unaweza kutazama na ulione, bali yakubidi uwe nalo ndani humu ukiangalia namna hii. Siyo nje huko ukitazama ndani, yakubidi uwe ndani ukiangalia nje. Unaona?

Huwezi kuja kwa kupitia hoja; huwezi kuja kupitia kwa haya mambo mengine; yakubidi ushuke kwa mkondo wa Mungu wa jambo hilo, moja kwa moja hadi kwenye nafsi. Nawe unalitendaje? Mkondo wa mwisho ni upi? Itaendelea kuhoji na kusema, "Hisi. Loo, na—naweza kulihisi. Ndiyo, hilo hapo. (A—haa.) Loo mimi, naweza kusikia harufu yake au na kadhalika. Mambo haya yapo, ndiyo."

Unajadili jambo jingine, "Vema, yaonekana yampasa kujua ambalo analizungumzia. Daktari anasema siwezi kupona. Hilo lapaswa kuwa . . ."

Unaona? Papo hapo ume—umekosea. Huyo ni pepo anayesimama hapo. Huyo ni pepo anayeingiza mambo haya ndani yako; usiliamini. Haleluya! Neno la Mungu lilisema, "Mimi, zaidi ya yote nataka ufanikiwe katika afya." Hilo ni kweli. Wawezaje kuwa askari mzuri nje huko? Unaona. "Nataka ufanikiwe katika afya."

Hiyo hapo papo hapo, mikondo hiyo. Kama ukiifungua tu; usithubutu kuiachilia. Basi kama Shetani anaweza kupitia pale, aingie kwa dhamiri hizi na mambo haya yote, basi anafikia moja kwa moja chini hapa mwisho wa nafsi katika akili. Naam, kama anaweza tu kukupata . . . Kamwe huta—kamwe hutaangalia hata moja yao mpaka kwanza umemruhusu aingie humu ndani. Yabidi umruhusu aingie; ndipo anapoingia ndani, ametawala.

Basi anafanya nini? Anaanza kutumia dhamiri. Anaanza kutumia *hili*, anaanza kutumia njia hii. Ni nini? Kuona, kuonja, kuhisi, kunusa, kusikia, mawazo, dhamira, kumbukumbu, hoja, upendo; anaanza kutumia mikondo yote hiyo midogo mbalimbali, maadamu angeweza kuingia ndani juu ya hii hapa. Lazima aje kwenye akili yako kwanza, na yakupasa kukubali. Huenda . . .

Sikiliza! Anaweza kukugongagonga, lakini hawezi kukufikia mpaka ukubali. Wakati Shetani alipomwendea Hawa na kusema, "Unajua, tunda lile linapendeza," alisimama kwa muda kidogo. Loo, hapo ndipo alipofanya kosa —wakati aliposimama kwa muda kidogo. Usisimame kwa jambo lo lote! Unao Ujumbe! Yesu yu hai; Mungu ndiye mponya; huo ndio Ujumbe. Usisimame kwa cho chote, wala hoja, wala cho chote kile.

Bali yeye alisimama kwa muda kidogo. Hapo ndipo ambapo Shetani alipotembea moja kwa moja kuingia katika akili yake. Akasema, "Vema, linaonekana kuwa ni jambo zuri." Loo, usifanye hivyo! Chukua tu alichosema Mungu.

Ibrahimu, vipi kama angelisimama kuhojiana wakati Yeye alipomwambia atapata mtoto kwa Sara, naye alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano na yeye sabini na mitano! Naye alipokuwa na umri wa miaka mia moja na yeye alikuwa na—na yeye tisini, yeye bado, alikiri kwamba Neno la Mungu ni kweli; naye aliita mambo hayo ambayo hayakuwepo kana kwamba yalikuwepo. Unaona? Yeye—yeye hata tumaini. Kulikuwa na tumaini lo lote? Hata hakutumia tumaini.

"Vema," unasema, "natumaini naweza kuwa mzima. Natumaini nitakuwa mzima. Natumaini nitapata Roho Mtakatifu. Natumaini mimi ni Mkristo. Natumaini nitafanya *hili*." Wewe hutaki hilo! Ibrahimu kamwe hakuangalia hilo hata! Amina! Pasipo matumaini yeye bado aliamini Neno la Mungu! Imani iko zaidi ya tumaini. Imani hutokea nyuma huku upande wa ndani, imani inatoka humu. Anaingiaje ndani? Kupitia akili hii, huu—mlango huu, mstari wa mbele wa vita akisimama pale.

Sasa, mpango wa vita unapokamilika . . . Naam, Ibilisi ameketi kwenye kila moyo asubuhi hii. Ameketi katika moyo wa msichana huyu mdogo; ameketi katika mioyo yenu; amekaa kila mahali pale. Alisema, "Loo, nimeliona likijaribishwa hapo kabla; nimesikia hilo hapo awali." Mtoeni nje; hilo tu, mtoeni

nje. Biblia ilisema nini hapa, katika somo letu? Mtoe nje; hilo ni sawa, mtoeni nje.

Tumefundishwa, nadhani, "Hivi sisi wahubiri tuna shida gani?" Sijui tumepata mafunzo ya namna gani. Mafunzo ya Mungu kwa vita hivi vikuu.

Mathayo 24 inasema kutakuwa—na pia Danieli 12 inasema kutakuwa na wakati wa dhiki mfano wake haukuwapo duniani hapo awali. Nasi tunaishi kwenye wakati ule ambapo utamaduni, na elimu, na kadhalika vimekaba Neno la Mungu na kuingia katika mahojiano na kadhalika. Vita vinapiganwa hivi sasa. Ni nani atakayesimama? Haleluya! Vita viko tayari kuanza; vimeandaliwa sasa.

Angalia ni upinzani mkubwa jinsi gani tulio nao kule. Ni nani atakuwa kama Daudi aliyesema, "Mnasimama na kumwacha Mfilisti huyu asiyetahiriwa ayatukane majeshi ya Mungu aliye Hai! Nitaenda nipigane naye." Amina! Mungu anataka mwanamume na mwanamke asubuhi hii ambaye anaweza kusimama na kusema, "Nitaamini Neno asemalo Bwana! Amina! Haidhuru nani ameshindwa, ambapo huyu ametenda na ambalo yule ametenda; hilo halihusiani nalo. Enyi akina Sauli na kadhalika, kama mnamwogopa, rudini nyuma makwenu, bali jeshi la Mungu linasonga mbele." Amina! Mashujaa, watu wenye—wenye imani, watu wenye nguvu, watu wenye akili. Si lazima wawe werevu; si lazima wawe na elimu; yawabidi wawe ile mikondo. Mungu huchukua mikondo hiyo midogo. Yeye alisimama kidogo kuhoji, akisema, "Vema sasa, hebu tuone."

Vema, kama vile tu . . . Vipi kama yule—mama huyu mdogo asubuhi hii, hapana shaka kwamba daktari amemwambia anakaribia mwisho wa maisha yake; hakuna kinachoweza kufanywa. Vema sasa, huyo—daktari huyo, simlaumu. Mtu huyo ni mwanasayansi. Ameona kwamba ugonjwa umeushinda mwili wa mtoto. Hautibiki. Hana dawa ambayo itaukomesha. Vivyo hivyo ile kansa ilimshinda mwanamke yule. Hakika, kifo kilikuwa kimemshinda mtoto yule, bali Kapteni wetu Mkuu (Haleluya!) wa jeshi hili kubwa, Yeye ndiye Ufufuo na Uzima; hakuna kinachoweza kumshinda Yeye. Haleluya!

Ubongo wa jeshi uko katika makapteni wake, akili. Rommel huko Ujerumani alikuwa ndiye ubongo wa Ujerumani—siyo Hitler, Rommel. Hiyo ni kweli. Eisenhower, mwanajeshi, Patton, hao watu ambao walikuwa vitani, inategemea jinsi walivyotoa amri.

Unamfuata kapteni wako. Kama yeye ni jenerali anayefaa, kama anafaa, kama ni jenerali mwenye nyota nne, kama amehakikishwa, kama amehakikishwa kuwa anafaa, mfuate! Ingawa yaweza kuonekana si sahihi kwako, songa mbele vitani; fanya kama yeye alivyokuambia! Haleluya!

Tunaye Jenerali mwenye nyota tano inayoendelezwa J-E-S-U-S, akiweka nyota tano juu yetu I-M-A-N-I. Hajashindwa vita kamwe. Haleluya! Yeye ameshinda mauti, kuzimu, na kaburi. Ondoeni pepo njiani. Yeye ndiye yule Kapteni Mkuu. Hivyo ibilisi hayupo hata kwenye picha.

Vita vikuu sana vilivyowahi kupiganwa viko tayari sasa hivi. Hakika viko tayari. Loo, Haleluya! Ninapoliwazia hilo, niliposimama pale na kumwona Yeye akifanya mambo, kumwona Yeye akiyafunua mambo, akiyafungua mambo, akisema, "Itakuwa jinsi *hii* na jinsi *ile,*" na ndivyo hivyo! Loo, kutazama nyuma hapa na kusema, "Ni nani huyu Kapteni mkuu?" Loo, sitazami nyuma kuona kama ni Daktari *Fulani*. Ninaona ambalo Kapteni alisema; Yeye ndiye Kapteni wa wokovu wetu. Heleluya! Wokovu ni nini? Ukombozi! Utukufu! Yeye ni Kapteni wa ukombozi wetu!

Saa muhimu ya "Shambulia!" imewadia. Haleluya! Askari aliye na silaha zinazong'aa, bendera zinapepea. Imani na shaka vimejipanga tayari kwa mapambano katika maskani hii asubuhi hii —shaka upande mmoja, imani upande mwingine. Enyi askari, simameni mahali mlipoamriwa! Haleluya! Kapteni wetu, Nyota ya Asubuhi anaongoza. Harudi nyuma kamwe; Yeye kamwe—hajui neno kumkimbia adui. Haimbidi *kumkimbia adui*. Amina! Hakika!

Vita vikuu sana vilivyowahi kupiganwa, vinaendelea mumu humu ndani sasa (ndiyo, bwana!) kati ya uzima na mauti, kati ya maradhi na afya, kati ya imani na shaka, (loo, jamani!) kati ya uhuru na utumwa. Vita vinaendelea. Ng'arisheni mikuki yenu, enyi askari, safisheni silaha.

Mungu anawatayarisha askari Wake. Amina! Mungu hupaka mafuta jeshi Lake. Marekani huvalisha askari wao vizuri kadiri wanavyoweza kuwavalisha, kofia za chuma, na dirii, na cho chote walicho nacho, vifaru vyenye silaha, na cho chote wanachoenda nacho. Mungu huvalisha jeshi Lake. Haleluya! Tunatumia zana za aina gani? Roho wa Upanga, Neno la Mungu. Amina! Neno la Mungu ni kali kuliko upanga wenye makali kuwili (Waebrania 4) huchoma hata kugawanya mifupa, hata ma—mafuta ya mifupa, hata—huyatambua mawazo ya moyo, Neno la Mungu. Kuamini Neno Lake, na hivyo ndivyo ambavyo Mungu huvalisha silaha.

Hilo ndilo Yeye alimpa Hawa ajivike, naye akavunja silaha yake. Aliivunjaje? Kwa kufungua akili yake kuhoji. Huhojiani na Neno la Mungu, Halina hoja. Wewe tu—Neno la Mungu tu. Hakuna—hakuna shaka kuhusu Hilo; hakuna kuhojiana Nalo. Ni Neno la Mungu, hilo latosha. Jambo ndilo hilo. Hilo latosha milele. Unaona ninalomaanisha, Mpenzi? Neno la Mungu. Mungu aliliahidi. Mungu alisema hivyo.

Walimwambia Ibrahimu, "Unajuaje utapata mtoto yule?"

“Mungu alisema hivyo!” Hilo lilitosha.

“Vema, mbona hunaye?”

“Sijui nitampata lini, lakini nitampata. Mungu alisema hivyo. Hilo halitanizuia hata kidogo!” Alikamata . . .

“Kwa nini usirudi nyumbani kwenu ulikotoka?”

“Mimi natakiwa kuwa msafiri na mgeni katika nchi hii.” Amina . . .? “Mungu alitoa ahadi; Mungu atanipa mtoto papa hapa kwenye nchi hii ambapo Yeye amenipeleka.”

Haleluya! Mungu atakuponya papo hapa katika uwepo huu wa Roho Mtakatifu, ambapo Yeye alikupeleka. Mungu atakupa hilo; liamini tu! Amina. Fungueni hayo mabomba ya nafsi na mwili, hisi na dhamiri, na . . . Hebu ruhusu maneno ya Mungu yapenye. Kwanza chukua hiyo akili; hapo ndipo penye uwanja wa vita. Siyo ati useme, “Vema, kama ningeweza kulihisi . . . Kama ningehisi utukufu wa Mungu ukishuka . . . ” Loo, hilo halihusiani nalo, hata kidogo. Fungua hiyo akili, huo ndio uwanja wa mapambano; hapo ndipo ambapo vita hujipanga, papa hapa kwenye mstari wa mbele, akili yako. Ifungue ukaseme, “Na . . . Kila shaka, natilia shaka mashaka yangu.” Amina! “Ninatilia shaka mashaka yangu sasa; ninaamini Neno la Mungu. Hapa naja, Shetani!” Kitu fulani kitatukia. Hakika kitatukia. Ndiyo, bwana!

Huwatia mafuta watumishi Wake kwa Roho Wake; Yeye huwapelekea malaika. Watu hucheka jambo hilo wakati mwingine, malaika. Hebu ni—hebu tu nifungue mahali fulani hapa pamoja nanyi kwa muda kidogo. Hebu tufungue Waebrania dakika moja, Waebrania sura ya 4. Sura ya nne, na hebu—ninamaanisha sura ya 1 ya Waebrania, na tufungue aya ya 14:

> *Je! . . . hao si roho watumikao* wakitumwa—*kuwahudumu wale watakaorithi wokovu?*

Je! yuko malaika ambaye Yeye alimwambia, “Uketi mkono Wangu wa kuume”—malaika wote wa Mungu.

Sasa, hapa Biblia inarudi na kutuambia hapa kwamba Mungu hupeleka malaika. Utukufu! Wao ni nani? Roho watumikao. Utukufu! Roho wanaotumika wanatumwa wapi? Toka Uweponi mwa Mungu. Kufanya nini? Kuhudumu Neno Lake. Amina! Hupaswi kuhudumu theolojia fulani ya kundi la madhehebu fulani, bali kutumikia Neno Lake. Hao ni Roho Wake watumikao waliopelekwa.

Tunajuaje wamepelekwa? Biblia ilisema kwamba Neno la Bwana liliwajia manabii. Sivyo? Malaika hawa huhudumu Neno Lake kwa Roho Wake, kuhudumu Neno kwa Roho Mtakatifu; na Roho na Neno viliwajia manabii; nao manabii walikuwa na Neno la Mungu. Hiyo ndiyo sababu waliweza kutenda ile miujiza waliyotenda. Haikuwa ni yule mtu, ilikuwa ni yule Roho wa

Mungu katika yule mtu, Roho wa Kristo katika mtu huyo. Kwa maana Neno la Mungu . . .

Alifanya nini? Alisafisha kila mkondo. Mungu alikuwa amemchagua, naye alikuwa ametiwa mafuta na Roho Mtakatifu, na haikuwa ni yeye. Yeye hakutenda neno mpaka alipoliona kwenye ono. Eliya alisema Mlimani Kameli, "Yote haya nimeyatenda kwa amri Yako. Sasa, Bwana, na ijulikane kwamba Wewe ni Mungu." Loo, Mungu atukuzwe.

Nimeliona mara nyingi sana. Unapoona Roho wa Mungu akishuka mahali fulani, na mahali hapo pakawa chini ya upako. Kama kundi hili dogo hapa asubuhi hii lingeweza tu kuchukua akili hii hapa, liondolee mbali kila shaka. Unawezaje kutia shaka tena unapoona wafu—wafu wakifufuliwa, viwete wakitembea, vipofu wakiona, viziwi wakisikia?

Malaika wa Bwana, hata picha Yake inaning'inia hapa kwenye ukuta, imeitia bumbuwazi sayansi kila mahali. Yeye anafanya nini? Anadumu tu katika Neno. Amina! Hukata kila pepo. Ndiyo, linakata. Ni nini? Roho watumikao waliopelekwa toka Uweponi mwa Mungu kuwatia mafuta wanenaji wa Neno, ambao wanakaa na Neno, Naye analithibitisha Neno kwa ishara zinazofuata. Anamleta Yesu yeye yule jana, leo, na hata milele. Huyo hapo.

Tungewezaje kuona shaka wakati Yeye kisayansi, kimaumbile, kiroho, kila njia ambayo yaweza kuthibitishwa, Yeye amethibitisha hapa. Kuna shida gani? Ni katika akili zetu. Tunafungua akili zetu kwa mambo, tunasema, "Vema, si—sijui iwapo ingewezakana au la. Labda, iwapo nitajisikia mzima zaidi kesho . . . " Loo, hilo halihusiani nalo kamwe.

Kama nilivyosema mara nyingi, pengine Ibrahimu angemwambia Sara . . . Amepita umri wa—wa kuwa mwanamke (wajua ninachomaanisha?), muda wa uhai, zile siku zake ishirini na nane. Unaona? Yeye alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano; pengine alikuwa ameupita kwa miaka kumi na mitano, ishirini. Naye akamwambia, pengine siku chache zinazofuata akasema, "Unajisikia tofauti kidogo, Mpenzi?"

"Hata kidogo."

"Hilo halihusiani nalo kamwe; tunaendelea mbele kwa vyo vyote. Vema sasa, ukianza kurudi kama mwa—mwanamke kijana tena, tunajua hilo kwa damu hiyo ya uhai, vema basi, tunaona hapo kwamba itamfanyia makazi mtoto mchanga na kila kitu kitakuwa sawa. Sasa, unajisikia tofauti kidogo leo? Imetimia mwezi mmoja tangu Yeye aliponiahidi mimi. Unajisikia tofauti kidogo Mpenzi?"

"Hata kidogo, Ibrahimu. Hakuna hata dalili, hakuna kitu. Ni—ningali niko tu sasa vile ni—nimekuwa kwa miaka michache iliyopita; hakuna tofauti hata kidogo."

"Mungu atukuzwe, tutampata haidhuru!"

Unamaanisha, Ibrahimu, kwamba . . . Angalia, iwapo Yeye alikuahidi wewe, hakika Yeye angetupa ishara namna hii. Kweli Yeye angetupa ishara!" Ha! Haleluya!

Kizazi kinyonge na cha zinaa chataka ishara. Hiyo ni kweli! Yeye alikuwa na ishara. Ilikuwa ni ipi? Neno la Mungu, Hilo lilikuwa ni Ishara. Mungu angewezaje kumponya mtoto Wake? Neno la Mungu lilisema hivyo. Kama nikisikia mshtuko au hakuna mshtuko, kama—haidhuru jambo gani linatukia, Mungu alisema hivyo, na hilo latosha.

Ibrahimu alisema, "Kusanyeni kofia zenu na kila kitu pamoja, tunaenda zetu kwenye ile nchi."

"Mnaenda wapi?"

"Mimi sijui (Amina!), bali tunaenda haidhuru. Hima twende!" Walifungasha wakaenda. Haleluya! Hilo ni Neno halisi la Mungu. Alishikilia nini mbele yake? Ahadi ya Mungu, Neno la Mungu. "Tutampata."

"Toka katikati ya watu wako, Ibrahimu, wao ni—jambo lenyewe ni kwamba wao ni wenye shaka na wasioamini, na watakutia kwenye mashaka yayo hayo. Toka ukajitenge nao uniishie Mimi." Ni jambo gani? "Achana na dhamiri zako, na hisi, na ishara ambazo wewe—namna hiyo; fungua akili yako, na ukumbuke ni Mimi. Njoo ukaishi pamoja Nami." Amina!

Mungu anaita kila Mzao wa Ibrahimu asubuhi hii kwenye maisha ya aina ile ile. Vita vikuu vinaendelea sasa, ulimwenguni mwote. Mungu anataka watoto wake wajitenge na nini? Kuona, kuonja, kuhisi, kunusa, kusikia, mawazo, dhamiri, kumbukumbu, hoja, upendo, kila kitu. Wafungue akili zao waruhusu Neno liingie ndani na watembee pamoja na Neno. Huyo ndiye askari halisi.

Hivyo ndivyo jinsi nyota zinavyosimama. Mfumo wa jua haujabadilika. Zodiaki, nyota ya asubuhi huchomoza katika wajibu wake kila asubuhi jinsi ile ile tu ilivyofanya wakati dunia ilipoumbwa. Nyota ya jioni huchukua mahali pake. Kila nyota, kundi dogo la nyota—katika majira yake lipo pale pale tu linapopaswa kuwa. Nyota ya Kaskazini husimama imara na haisogei kamwe. Haleluya! Zote huzunguka Nyota ya Kaskazini—zingine zote, kwa sababu iko katikati kabisa ya dunia; huyo ni Kristo. Amina!

Yeye husimama pale, anaamrisha jeshi Lake kama Kapteni mkuu. Kama Musa juu mlimani akiwa ameinua mikono yake, na Israeli alikuwa anapigana, wakiwafyeka kufanyiza njia; naye alisimama huku ameinua mikono yake juu. Alisimama ameinua mikono yake juu mpaka jua likashuka; iliwabidi waishikilie mikono yake juu. Huyo alikuwa ni Musa; alikuwa mfano wa Kristo. Ili kuhakikisha kwamba mikono Yake inakaa juu,

mikono Yake ilipigiliwa misumari msalabani. Haleluya! Kisha Yeye akapanda ngome za Utukufu leo na mavazi Yake yenye damu mbele za Mungu kwenye mkono wa kuume wa Ukuu Wake huko. Na vita kwa kila askari atafyeka afanyize njia (Mimi sijali nini kitakachotukia) kwa Neno la Mungu, atakata hata ajiweke huru. Amina!

Kama vile kifaranga katika yai, itakuwaje kama yeye anaogopa kulia? Vipi kama anaogopa kudonoa lile yai? Vipi kama huyo kifaranga mdogo ndani ya yai, ndege mdogo aliogopa kugongagonga ganda la yai? Vipi kama angesikia sauti kutoka nje, ikisema, "Usigonge ganda hilo; huenda ukajiumiza mwenyewe"? Bali asili yenyewe katika ndege yule inamwambia, "Lidonoe! Toboa tundu katika hilo."

Acha madhehebu yote yale ya kale yaseme, "Siku za miujiza zimepita. Utajiumiza. Umeanza kuwa shupavu wa dini."

Donoa ganda kwa nguvu uwezavyo. Haleluya! "Shetani, simile; ninatoka humu ndani; silali hapa tena; sikai hapa tena; siko kwenye ardhi hii ya ibilisi ya kale tena; ninadonoa nipate njia ya kutoka asubuhi hii! Amina! Mimi ni tai!" Amina! Haleluya!

Kwa yule maskini tai mdogo, mwenye shingo la kijinyundo nyuma kule akidonoa kwenye ganda lile, haidhuru ganda lile lilikuwa ni gumu vipi, alililidonoa akalitoboa kabisa. Muda si muda aliweza kutapatapa kwa mbwawa zake kidogo. Alikuwa sawa.

Donoa utoke; hiyo ni kweli. Unalifanyaje? Kulilipua na BWANA ASEMA HIVI, BWANA ASEMA HIVI, BWANA ASEMA HIVI; hatimaye anaanza kunusa hewa safi. BWANA ASEMA HIVI—umetokeza kichwa chako nje. BWANA ASEMA HIVI. Sukuma kwa nguvu sasa, unatoka! Harudi kamwe tena kwenye ganda. Amina! Yuko huru. Loo, jamani! Neno lile, likisha tu kuwekwa chini kupitia hisi hizo zote, na dhamiri, na kadhalika, hadi Hili litulie chini hapa, na akili hiyo inafunguka na kuliruhusu (ee Mungu, uturehemu), hakuna kamwe kitu cha kumtia utumwani tena. Uko huru. Yeye ambaye Mwana amemfanya huru yuko nje ya ganda.

Madhehebu yako hayawezi kamwe kukuita urudi; ibilisi hangeweza kamwe kutenda cho chote zaidi kwako; anakufanyia mlio wa nyoka na kukuzomea, bali uko kwenye njia kuu ukikimbia kasi. Loo jamani, ukikimbia kwenye njia kuu ya Mfalme, askari mtiwa mafuta wa msalaba. Enyi tai wote mlio na imani tangazeni "Yesu Nuru ya ulimwengu," kimbieni katika njia kuu ya Mfalme.

Hakika! Ndiyo, bwana! Hawa ni Roho watumikao waliopelekwa toka Uweponi mwa Mungu kuwa wahudumu. Kuhudumu nini? Neno Lake —sio theolojia fulani, bali Neno la Mungu. Wao ni Roho watumikao waliotumwa kutoka kwa

Mungu kuhudumu, Roho watumikao. Loo! Basi kumbuka kama akihudumu kitu fulani kando ya Neno, hakutoka kwa Mungu, sababu Neno Lako sikuzote linathibitishwa Mbinguni. Sikuzote Mbinguni, Neno, Mungu huliangalia Hilo, Naye hatampeleka kamwe Roho kuhudumu kitu fulani nje ya Neno.

Yeye hatampeleka kamwe Roho mwenye D.D.D., Ph.d. kubwa, huku ukosi umepinduliwa nyuma na mambo kama hayo, aseme, "Vema, bila shaka, siku za miujiza zimepita. Sote tunajua hilo." La, la! Hilo halikuja kutoka kwa Mungu, ni kinyume cha Neno. Amina! Yeye huwapeleka wale ambao huhudumu Roho wa Neno. Amina. (Loo, nilikuwa na mambo kama manne au matano zaidi, bali nitaacha hilo lipite wakati huu, nitaendelea nalo Jumapili ijayo. Sawa!)

Shetani na pepo wake wametiwa mafuta. Kama Roho hizi za malaika zimetiwa mafuta kuwaleteeni Neno, kuwafanya muamini Neno . . . Sasa, umepata kuona ambapo umewahi kusikia nabii, nabii halisi wa Mungu akikana Neno la Mungu? La, bwana! Ilikuwaje hapo madhehebu ya nyakati zao yalipoinuka na kusema, "Sasa, yeye amekosea." Alisimama peke yake na akasimama pekee. Alisema, "Ni kweli."

Mwangalie Mikaya chini huko siku ile, maskini mtakatifu anayejifingirisha (unaona?), mwana wa Imla. Palikuwa na mia nne waliotiwa mafuta—walivyodhaniwa—manabii waliotiwa mafuta wamesimama pale wote wamelishwa vizuri, na kuwekwa vizuri na shahada kubwa, na elimu kem kem na wanachuoni walioadibishwa, akasema, "Kwea, mfalme wetu mwaminifu. Bwana awe pamoja nawe. Hiyo ni yetu; Yoshua alitupa sisi, kwa hiyo kwea ukaitwae. Hilo ni kweli kabisa. Kwea ukaitwae."

Alisema nini, "Vema, Yosh—" Unajua, Yehoshafati akasema, "Je! hayupo mwingine mahali fulani?" Vema, walikuwa na mia nne; kwa nini asiamini wale mia nne. Akasema, "Lakini hakika, mna mwingine mahali fulani."

Akasema "Ni—ni . . . Naam, tunaye mmoja. Kuna mwingine, bali, loo, namchukia."

"Papo—hapo, huyo ndiye jamaa ningependa kumsikiliza." Unaona? Akasema, "Mleteni. Hebu tuone atasema nini."

Na kwa hiyo walienda wakamwambia, wakasema, "Sasa sikiliza! Wewe panga mahubiri yako barabara asubuhi hii, sababu unamhubiria mfalme. Unahubiria cha—chama cha wahudumu wa *Fulani na fulani* (unaona?) wa Palestina, chama chote cha wahudumu. Naam, kumbuka, hivi ndivyo walivyosema; wewe nena jambo lile lile; amini jambo lile lile."

Maskini huyo . . . Yeye—yeye alipata mtu asiye pale! Mtu yule aliisha achana na akili hii ya kale yenye kuhoji. Alikwisha safisha lile bomba (unaona?), dhamiri zake, na . . .

"Naam—naam, unajua watafanya nini? Kama utasema jambo lile lile, nadhani watakufanya kiongozi wa kanisa wilayani; pengine watafanya hivyo. Wata—watakufanya mwangalizi wa mambo yote ya humu wilayani kama uta—kama utakubaliana nao." Huyo hakuwa mtu wa Mungu halisi.

Mbona, mabomba yake yalikwisha safishwa, dhamira zake zote na kila kitu wazi; akili yake iliisha funguka kwa ajili ya Neno la Mungu; naye angeamini Neno la Mungu pekee. Hao ni Roho watumikao; huyo ni Roho atumikaye. Akasema, "Sijui la kusema sasa, bali nitawaambieni jambo hili moja: nitasema tu kile Mungu ataniambia niseme." Kwa hiyo wakangojea usiku ule; naye akaona ono.

Asubuhi iliyofuata, naweza kuwazia Mikaya akiyachunguza Maandiko na kusema, "Sasa, hebu tuone sasa. Hivi ono lile... Naam, watu hao wote...Kuna kasoro fulani mahali fulani hapa, sababu ni kinyume cha walilolisema. Bali lingesema nini Hilo? Hebu na tuone ambalo Eliya alinena huku nyuma, yule nabii, sababu tunajua alikuwa nabii. Tuone ni Neno gani la Bwana lililomjia Eliya, ndiyo, Nalo lilisemaje? 'Kisha mbwa watalamba damu yako, Yezebeli. Mbwa watamla, na—sababu ya Ahabu mwenye haki—mwenye haki Nabothi.'" Akasema basi...Alipoona hilo, alipoona kwamba ono lake lilipatana na Neno la Mungu. Hapo ikawa maskini mzee Ahabu ataona cha mtema kuni.

Aliondoka akaenda hadi pale akasema, "Kwea, bali nimemwona Israeli..." Unaona, hakuona haya kusimulia ono lake basi, sababu lilikuwa Neno la Bwana. Alijua angeweza kuchukua jambo lile kikamilifu. Ni nini? Alikuwa ameufungua moyo wake na akili zake kwa Neno la Mungu, na Neno la Mungu lilikuwa limeisha kufunuliwa kwake, kwa hiyo alijua hilo lilikuwa Neno la Mungu kabisa.

Sasa, unasema, "Loo, laiti ningelikuwa Mikaya!" Unaweza kuwa; ndivyo ulivyo! Ndivyo ulivyo pia, Mpenzi. Wewe u Mikaya, yule nabii. Utafanya nini? Fungua akili yako. Ninajaribu kukuambia nini asubuhi hii? Neno la Bwana. Unaona? Fungua akili yako; useme, "Sasa, unajua, ninaamini ninaweza kuponywa."

"Vema, ni nini basi? Ni Neno la Bwana?"

Hakika Hilo ni Neno la Bwana! Na mtu huyu hapa anasema, "Siku za miujiza zimepita; huwezi kutenda hili..." Sahau hilo! Mweke Mungu kwanza! Hili hapa Neno la Bwana linakuja, naye alilinena, Nalo likawa.

Sasa, Shetani alifanya nini? Shetani aliwatia mafuta wale wengine. Naam, Shetani hutia mafuta watumishi wake. Loo hakika, a-haa, hakika! Huwatia mafuta watumishi wake. Anawatia mafuta na nini? Na kutoamini. Shetani na pepo wake

huwatia mafuta binadamu wasiliamini Neno la Mungu. Sasa, ukitaka kuthibitisha hilo, fungua Mwanzo 3:4.

Hebuni tufungue nyuma kule tusikilize hili kidogo, tuone kama hiyo siyo mbinu yake ya kwanza. Hilo ndilo jambo la kwanza alilotenda; kamwe haachi mbinu zake zile zile; hutenda hilo wakati wote. Naam, hebu angalia kama ndivyo—ndivyo ilivyo. Sasa, hakulipinga Neno; kwa namna fulani alimfanya aelewe hilo vibaya kidogo tu, unajua, kwa namna fulani kulifanya Hilo lisikike jinsi alivyolitaka Hilo lisikike—usichukue Neno zima. Sasa, Mwanzo, nimepata hapa Mwanzo 3 na 4. Hebu tuone kama hivyo ndivyo linasema sasa. Sawa.

Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa,

. . .*hakika hamtakufa*, unaona jinsi alivyolinukuu vinginevyo? “Loo, tunaamini siku za miujiza zimepita. Hatuamini kuna kitu kama watu kupokea Roho Mtakatifu kama walivyofanya kwenye Pentekoste. Loo, namna yo yote ubatizwayo, haileti tofauti yo yote.” Unamwona huyo ibilisi? Unaona mbinu zake?

“Vema, kama daktari amekuambia huwezi kupona, hilo latosha.”

Naam, si kumvunjia heshima—kutokumwamini daktari, daktari anatenda kazi katika njia ya kisayansi. Na daktari amefanya kila awezacho kuokoa maisha ya mtu yule; na hayawezi kuokolewa, kwa sababu hakuna kitu kingine ajuacho kutenda; amefikia kikomo cha akili zake. Huyo mtu ni mwaminifu.

Bali sasa, ule mti wa maarifa ni sawa, bali unapofikia kikomo chake, basi nenda kwenye Mti wa Uzima na kusonga mbele. Amina. Ndivyo hivyo. Itafanya tu kazi umbali huo. Ndiyo!

Sasa, hizi mbinu za Shetani zinafaa nini sasa? Inasema nini hapa? Sasa angalia, ya kwanza na a—aya ya 2. Naam, hebu—hebu nisome aya ya 1 hapa hadi ya 3.

Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wote—wanyama wote wa mwitu aliowafanya BWANA Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile . . .matunda ya miti yote ya bustani?

Msikilize sasa, jinsi tu anavyochukiza na jinsi yeye—jinsi anavyolipaka hilo Neno chokaa. Unaona? Anajaribu kufanya nini? Kuingia akilini mwake. Unaona? Anazungumza naye baada ya Neno kufanya ngome mle. Sasa, usimwachilie Shetani afanyie ngome cho chote. Unaona? Wewe lifanye ngome Neno la Mungu moyoni mwako. Unaona? Fanya jambo lilo hilo. Sasa angalieni, ninyi akina Mikaya.

Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula;

> Bali ma—*Lakini matunda ya mti ulio katikati...* (katikati, mnaona?) *ya bustani, Mungu...amesema, Msiyale, wala msiyaguse, msije mkafa.*

Unaona? Sasa, hilo ni Neno; anamnukuulia hilo. Sasa angalia!

> *Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa,*

Unaona mbinu zake? Unaona? Anajaribu kufanya nini? Yule mwanadamu wa kwanza, anajaribu kumtia mafuta yule mwanamke wa thamani pale, binti wa Mungu, kwa kutokuamini katika Neno la Mungu. Hilo ndilo hasa analojaribu kumfanya atende. Hilo ndilo ambalo angejaribu kukufanya utende, Mpenzi. Hilo ndilo ambalo angejaribu kumfanya kila. mmoja wenu kutenda huko nje—kukutia mafuta. Na kitu pekee kikupasacho kutenda (sasa, wewe u kiumbe chenye hiari; naam, unaweza kulikubali ukitaka), bali lipige teke!

Laiti Hawa asingalisimama muda ule kusikiliza! Usisimame kamwe! Usisimame!

Wakati yule—wakati Eliya alipomwambia Gehazi, kasema, "Chukua fimbo yangu, nenda uiweke juu ya mtoto aliyekufa; na kama mtu ye yote hata akikuzungumzia, usimjibu. Mtu ye yote akijaribu kukusimamisha, wewe endelea kusonga mbele!"

Mwangalie yule mwanamke alipomwita mtumishi wake. Alisema, "Jitandikie nyumbu unitangulie, na hata usisimame mpaka nitakapokuambia." Naam basi. Ukiwa na Ujumbe, endelea mbele. Amina! Kasema, "Siwezi kutembea. Ndiyo naweza. Sasa—loo, ninadhoofika." Endelea tu mbele; usisimame! Ukiweka kando kila kitu, endelea kufyeka upate njia. Ndugu, unao Upanga mkononi mwako, endelea tu kukatakata.

Nilikwenda kwenye uwanja wa kandanda wakati mmoja na nilikuwa naenda kuhubiri, nami nikasimama mlangoni na kutazama juu, juu kule, na kuliandikwa, "Si ukubwa wa mbwa katika mapambano, ni ukubwa wa mapambano katika mbwa." Kwa hiyo hicho ndicho kinachoshinda vita. Unaona?

Unasema, "Vema, tazama—tazama makanisa yote makubwa yako kinyume cha hili." Sijali ni makubwa kiasi gani, ni lile pambano ambalo limo ndani ya mbwa, hilo ndilo lenye maana. Ni ile imani iliyomo ndani ya mtu binafsi. Kama wewe u mwoga, rudi tunduni ukajikunyate. Vema, Ndugu, iwapo wewe ni askari, simama nje huko; vita vinaendelea. Kweli na uongo vinapambana. Hebu tupigane.

Kama Peter Cartwright alivyoingia katika jiji fulani, akasema, "Bwana aliniambia mimi ni—nije hapa na kuanzisha ufufuo." Akakodi stoo ya zamani, akaingia humo, akaanza kuisafisha.

Basi jitu moja katili la lile jiji, huku bastola inaning'inia ubavuni mwake, lilishuka likachukua . . . milango . . . Baadhi yao wakasema, “Yule jamaa anafanya nini chini kule?”

Wakasema, “Ni mhubiri. Alisema anataka kufanya mkutano.”

“Vema,” akasema, “naona itanibidi nishuke niende nikamtupe nje barabarani, nimfukuze atoke humu. Hivyo tu. Hatutaki mikutano yo yote kwetu.”

Hivyo anashuka anaenda huko na kusimama mlangoni; na Peter Cartwright amevaa koti lake, unajua, naye alikuwa tu anasafisha madirisha na kuta—kijitu kidogo, unajua. Yule mhubiri wa zamani alimcheka, unajua, kwa kula kuku kwa mikono yake (jambo ambalo ni kawaida leo, unajua). Kwa hiyo alikuwa tu anasafisha madirisha na kutengeneza kila mahali. Lile jitu katili likamwendea, likavuta nyuma koti lake, huku bastola imening'inia ubavuni mwake, kasema, “Unafanya nini?”

“Loo,” akasema, “ninasafisha madirisha.” Aliendelea tu kusafisha madirisha, unajua. Alikuwa na kusudi moja: Mungu alimwambia aende akaanzishe ufufuo. Akaendelea kusafisha madirisha . . .

Akasema, “Sisi haturuhusu ufufuo hapa.”

Akasema, “Loo, lakini Bwana aliniambia ni—nikaanzishe ufufuo huu.” Unaona? Aliendelea tu kujishughulisha na kazi yake. Unaona, unaona?

Akasema, “Kuna jambo moja linalokupasa—linalokupasa kufahamu.” Akasema, “Mimi ndiye ninayetawala mji huu hapa.”

Akasema, “A—haa, kumbe ni wewe unautawala?” naye aliendelea tu kusafisha madirisha, unajua.

Akasema, “Kabla ya kufanya ufufuo itakubidi unipige unishinde kwanza!”

Akasema, “Kumbe, ati inanibidi nikupige? Vema, nitafanya tu hivyo baadaye basi!” Akatoa tu koti lake, akaenda akamshika ukosini, akamtupa chini sakafuni, kisha akamrukia na kumkalia, akasema, “Sharti nipigane vita nipate kutawala. Zidisha ushujaa wangu, ee Bwana.” Akamtwanga akaona kilichomtoa kanga manyoya. Kasema, “Je! Umetosheka?”

Akasema, “Ndiyo.” Akasimama akampa mkono; aliokoka usiku ule kanisani. Ndivyo hivyo. Unaona? Chukua tu Neno la Mungu ufyeke upate njia kupitia kila shaka! Unaliona? Hakika, ndivyo ilivyo! Kama hiyo ndiyo kazi inayofuatia, hebu na tuifanye. Sawa! Jambo jingine ninalofanya ni kuondoka kwenye mashaka yangu, kuyakatalia mbali.

Hiyo ndiyo kazi yangu inayofuata ni kuondoa mahangaiko yangu. Kama hisi zangu zikiniambia, "Naam, wewe unaumwa," jambo la pili ni kukatilia kitu hicho mbali. Hilo ni kweli.

Unasema, "Vema, wewe—wananiambia kwamba a-haa... Unajua, dhamiri yangu yaniambia, Ndugu Branham, kwamba naweza..." Vema, afadhali ukatilie mbali jambo hilo; hutaenda mbali zaidi ya hapo. Fanya tu kazi yako inayofuata. Vua koti lako ukajiingize moja kwa moja kazini. Endelea tu kusonga mbele. Lengo moja: "Nitashinda." Amina! "Siwezi kushindwa. Nitashinda." Amina!

Shetani hutia mafuta. Unaona? Mbinu yake ya kwanza ni nini? Mahali pake pa kwanza kupafikia palikuwa ni wapi? Akilini. Mwanamke alisimama kwa muda kidogo kusikiliza alilosema.

"Loo, usiseme hivyo!" Hapo ndipo ambapo maskini wanawake wengi walipofanya makosa yao, na maskini wanaume wengi walifanya makosa yao. Hilo ni kweli. Kusimama kidogo, kusimama tu kidogo.

Mara ngapi nimeona kesi za talaka na mambo kadha yakizuka? "Naam, nakuambia, Ndugu Branham, alipiga mruzi kama [Ndugu Branham anafanya sauti kama ya mbwa-mwitu akipiga mruzi—Mh.] unajua, nami nikasimama; na kwa kweli, si—sikutaka kufanya hivyo." A-haa a-haa, naam basi.

"Loo, yeye...nilikuwa nimeketi upande wa pili wa meza toka alipokuwa; mwanamke—huyo mwanamke alikuwa na macho mazuri kupindukia." Unaona, unaona, unaona? Unaona? Haya basi. Ibilisi hufanya jambo lilo hilo.

"Loo, daktari aliniambia singepona, kwa hiyo mimi..." Haya basi. Jambo lile lile. Unaona? Vita vikuu sana vilivyowahi kupiganwa!

"Vema, wananiambia...Nilimwona *Fulani na fulani* wakidai kuwa wana Roho Mtakatifu..." Ndiyo, ulimwangalia maskini mnafiki fulani. Je! vipi kuhusu hao ambao kweli wanaye Huyo? Unaona? Ndiyo, ibilisi atakuonyesha maskini chambo fulani cha kunguru, bali hatakuonyesha hua halisi. Hiyo ni kweli. Hatakuonyesha huyo; atakupofusha usije ukamwona.

Loo, yeye ni shujaa pia. Kumbuka, bali aliye mkuu zaidi ni—aliye mkuu zaidi ni Yeye aliye ndani yako, kuliko yeye aliye katika ulimwengu. Kwa hiyo shikilia Neno la Mungu; liamini Hilo; enyi makapteni wa jeshi hapa. Shikilia ngome yako, Ndugu. Hiyo ni kweli, shikilia jukumu lako!

Basi, nilikuwa na msichana mdogo hapa wakati mmoja. Huenda huyo bibi ameketi hapa sasa; jina lake lilikuwa Nellie Sanders. Mojawapo ya mara za kwanza nilizowahi kuona pepo akitolewa. (Tuliishi katika...Sasa, kama ninaweza tu kupapata mahali pale katika—ingekuwa kama tu majengo

matatu juu hapa, kupita makaburini.) Sasa, ilikuwa ndiyo kwanza niwe mhubiri, nami nilikuwa na mkutano wa hema papa hapa pembeni. Na maskini msichana huyo alikuwa mmoja wa wacheza dansi hodari sana. Alisoma katika shule ya sekondari chini hapa. Naye na Lee Horn (na wengi wenu ninyi hapa mjini mnamjua Lee Horn, anaendeleza chumba cha kuchezea kamari kule)— kwa hiyo wao, yeye na Lee Horn, walikuwa ndio wacheza dansi hodari sana nchini. Yeye mwenyewe ni Mkatoliki; bila shaka, dini haikumaanisha kitu kwao. Kwa hiyo basi (Nellie na wengineo), kwa hiyo msichana huyo alikuwa mcheza dansi hodari sana na kijana huyo vivyo hivyo, nao walikuwa na dansi hii hapa inayoitwa "kitako cheusi" na "ngoma kasi" na kadhalika; naye alikuwa—hao wawili walikuwa ndio hodari sana nchini.

Siku moja alipepesuka akaingia humu (usiku mmoja) mkutanoni. Hapo akaanguka chini madhabahuni, maskini Nellie; namtakia heri. Alilala tu pale madhabahuni, aliinua kichwa chake, akalia; na machozi yakitiririka kwenye mashavu yake, akasema, "Billy . . . " (Alinijua.) Akasema, "Nataka sana kuokoka."

Nikasema, "Nellie, unaweza kuokoka; Yesu tayari amekuokoa, ewe msichana. Yakupasa uukubali sasa juu ya msingi wa Neno Lake." Naye akakaa pale, akalia, akaomba, na akamwambia Mungu hatasikiliza mambo ya ulimwengu tena. Mara, amani nzuri sana ikaingia nafsini mwake. Akainuka kutoka hapo akipiga makelele na kumsifu Mungu, akimtukuza Mungu.

Basi yapata miezi sita, au minane baadaye, alikuwa akishuka kwenye Barabara ya Spring usiku mmoja (sasa akiwa msichana mdogo, alikuwa tu katika umri wa tineja, kama miaka kumi na minane), naye akaja kwangu, akasema, "Hope . . . " (Huyo alikuwa mke wangu, yule aliyeaga dunia.) Akasema, "Laiti ningalifanana na Hope na Irene." Akasema, "Unajua, hawakuingia kamwe katika mambo ya ulimwengu." Kasema, "Ulimwengu unakutia alama." Kasema, "Nilipata sura ya kijeuri." Kasema, "Sasa niliacha kujipodoa na kadhalika, bali nina sura ya kijeuri. Hata sura ya uso wangu," akasema, "mimi naonekana jeuri." Akasema, "Wao huonekana wasio na hatia na wapole." Akasema, "Laiti nisingelifanya jambo hilo."

Nikasema, "Nellie, Damu ya Yesu Kristo husafisha dhambi yote, Mpenzi. Endelea, amini hilo."

Wayne Bledsoe (wengi wenu mnamjua hapa, rafiki yangu wa moyoni kwa miaka kadha wa kadha, alikuwa mlevi, naye alikuja hapa na ndugu yangu, Edward. Naye alilewa chini hapa barabarani, basi nikamwokota, sababu polisi wangemshika. Nami nikamleta juu hapa; nami nilikuwa mhubiri na niliishi juu hapa na mama na baba yangu kabla sijaoa. Basi nikamchukua,

nikamweka kitandani mle ndani; nililala—nililala kwenye kitanda cha watu wawili cha mkunjo. Kuna kundi kubwa la Wabranham, unajua (tuko watu kumi) na kwa hiyo tulikuwa na kama vyumba vinne, na ilitubidi kwa namna fulani tulale wawili-wawili kidogo. Kwa hiyo nilikuwa na kitanda cha watu wawili cha mkunjo nilicholalia; nami nilikivuta nje hivi na—na kumweka Wayne kitandani alale pamoja nami, amelewa. Ilibidi nimbebe humo nyumbani na kumlaza kitandani. Na nilipokuwa nimelala pale, nikasema, "Wayne, hivi huoni aibu ukiwa namna hiyo?"

Yeye, "A-haa, dah, Billy, usinizungumzie hivyo." Unajua? [Ndugu Branham anaigiza mlevi akizungumza—Mh.] Niliweka mkono wangu juu yake nikasema, "Nitakuombea, Wayne. Mungu akubariki."

Nami nimeokolewa kama, loo, nadhani kama, labda mwaka mmoja. Na kwa hiyo basi mara moja te—teksi, ikafungwa mlango huko nje, na mtu akapiga hodi kwa nguvu sana, "Ndugu Bill! Ndugu Bill!" [Ndugu Branham anagongagonga kwenye mimbara—Mh.]

Nikawaza, "Salala, lazima kuna mtu anayekufa." Nikaruka kwenda mlangoni, nikanyakua kitu changu kikuukuu pale, nikakizungusha kwenye pajama zangu namna hii, nikamfunika Wayne, nikakimbilia mlangoni. Ilisikika tu kama mwanamke. Nikafungua mlango, na kijana msichana huyu amesimama mlangoni, akasema, "Loo, naweza kuingia ndani?"

Nikasema, "Ingia," nami nikawasha taa na . . .

Sasa, alikuwa akilia namna hiyo, akasema, "Jamani, Bill—Billy, nime—nime—nimekwisha, nimekwisha!"

Nikasema, "Kuna nini, Nellie? Umepata u—ugonjwa wa moyo?"

Akasema, "La." Akasema, "Ndugu Bill, nilikuwa nikija kwenye Barabara ya Spring." Akasema, "Kweli, Ndugu Bill, kweli, Ndugu Bill, sikukusudia mabaya; sikukusudia mabaya."

Nikasema, "Kuna nini?" Nikawaza, "Nitafanya nini naye sasa?" Unaona? Sikujua la kufanya. Nilikuwa tu kijana, basi nikawaza . . .

Kasema, "Loo, Ndugu Bill," kasema, "niko tu—niko tu—nimechanganyikiwa kabisa."

Nikasema, "Sasa, tulia, Dada. Niambie yote kuhusu jambo hilo."

Basi akasema, "Vema," akasema, "nilikuwa ninashuka kuja barabarani, na Ukumbi wa Redmen . . . " (Basi walizoea kuandaa dansi ya Jumamosi usiku kule.) Naye akasema, "Nilikuwa na kitambaa; nilikuwa ninaenda nyumbani kujishonea nguo." Akasema, "Nilisikia muziki ule, na," akasema, "unajua," kasema, "nilisimama kidogo tu, na," akasema, "uliendelea

kuwa mzuri. Kwa hiyo nikawaza, ‘Unajua, haitadhuru kama nikisimama papa hapa.”

Hapo ndipo alipofanya kosa lake, alisimama kitambo kidogo.

Alisikiliza tu, akasema, “Vema, nitafikiria.” Kasema, “Ee Bwana, Wewe unajua ninakupenda. Loo,” akasema, “Wewe unajua ninakupenda, Bwana, bali ninaweza hakika kukumbuka wakati ambapo mimi na Lee tulikuwa tukichukua vi—vikombe vyote na kadhalika.” Kasema, “Jamani, ninakumbuka muziki ule wa kale ulikuwa unanivutia; sasa haunivutii.” Loo, loo! Loo, loo, unafikiri tu haukuvutii, tayari umekwisha kukushika papo hapo. Hilo ni sawa tu na anavyotaka papo hapo. Unaona?

Ni wangapi waliwahi kumjua Nellie Sanders? Vema, nadhani wengi wenu. Ndiyo, hakika! Kwa hiyo wao—wao walikuwa—akasema a . . . Akasema, “Vema, unajua nini?” kasema, “Labda kama nikipanda kwenye ngazi juu kule,” kasema, “labda nitaweza kuwashuhudia baadhi yao.” Unaona, uko moja kwa moja kwenye ardhi ya ibilisi. Usiikaribie! Epuka tu kule kuonekana kwa uovu!

Bali alipanda hadi juu ya ngazi na kusimama hapo dakika chache, basi muda si muda, wajua, alikuwa amekumbatiwa na mvulana fulani wanacheza dansi. Ndipo akajirudia, naye alikuwa amesimama pale akilia na kadhalika, kasema, “Loo, nimepotea sasa kabisa.”

Nikawaza, “Vema, sijui mengi mno kuhusu Biblia, bali ninaamini Yesu alisema hivi: ‘Katika Jina Langu watatoa pepo.’” Basi Wayne alikuwa amelevuka kidogo na alikuwa anaketi pale akiangalia jambo hilo. Unaona? Kwa hiyo nikasema, “Sasa, ewe pepo, sijui wewe ni nani, bali ninakuambia sasa, huyu ni dada yangu, nawe huna amri juu yake, kumshikilia. Yeye hakutaka kufanya jambo hilo; yeye alisimama tu kwa muda kidogo.” (Hapo ndipo ambapo hata hivyo alifanya kosa lake.) Nikasema, “Lakini itakubidi kutoka hapa. Unanisikia?” Na kwa hiyo nisaidie (Mungu atajua kwenye kiti cha hukumu), ule mlango wa kisetiri ukaanza kufunguka na kufunga wenyewe—pampiti, plampiti, pale mlangoni. Ka—plamp, ka—plamp, ka—plamp. Nikawaza . . . Naye akasema, “Bill, angalia kule, angalia kule!”

Basi nikasema, “Ndiyo. Hicho ni nini?”

Akasema, “Mimi sijui.”

Nikasema, “Wala mimi!” Na mlango unaenda pampiti, pampti, pumpu, ukijifunga hivyo, nikafikiri, “Kuna nini hapa? Kuna nini?” Nami nikachungulia ndani hivyo, nikasema, “Mwache, Shetani. Katika Jina la Yesu mtoke!” Niliposema hilo, ilionekana kama popo mkubwa mno, yapata urefu *huu*, aliruka kutoka nyuma yake, akiwa na nywele ndefu zikining’inia chini toka kwenye mbawa zake na kwenye miguu yake hivyo;

anakwenda, “Whrrrrrrr,” akaanza kuja upande wangu, kwa kasi kadiri alivyoweza. Nikasema, “Loo, Bwana Mungu, Damu ya Yesu Kristo inilinde na kitu hicho!”

Ndipo Wayne akaruka kitandani, akaangalia; hiki hapa kama kivuli kikubwa, kikazunguka, na kikaruka juu, na kwenda chini nyuma ya kitanda. Wayne akachomoka kitandani, akaingia chumba kingine mbio alivyoweza kukimbia.

Kwa hiyo sisi—nikamchukua Nellie na nikampeleka nyumbani, nikarudi, na sikuweza . . . Mama akaingia mle ndani na akakung’uta shuka na kila kitu; hapakuwa na kitu kitandani. Ilikuwa ni kitu gani? Pepo alimtoka! Kulitokea nini? Alisimama kidogo. Hiyo tu.

Usisimame hata kidogo! Mungu anapozamisha Neno Lake moyoni mwako, chukua tu Upanga huo na uanze kupasua na kukata! Haleluya! “Sina muda wa kungojea kitu kingine. Nimevuka tu hivi punde, sina hata muda wa kuketi nipumzike.”

Akasema, “Ukichukua fimbo yangu na kuiweka juu ya mtoto; na kama mtu ye yote akikuzungumzia, hata usimjibu. Kama ibilisi akisema, ‘Aisee, unajua unavyojisikia . . .?’ Hata usimzungumzie. Endelea kusonga mbele.”

Ibilisi—unajua, ibilisi anasema, “Lakini unajua nini? Unamjua *Fulani na fulani,* walipompokea Roho Mtakatifu, unakumbuka wao—karibu warukwe na akili.” Hata usimzungumzie; endelea kusonga mbele. Huna habari juu ya *Fulani na fulani,* ni wewe na Mungu. Hilo ni kweli. Mshikilie Mungu!

Yeye hutia mafuta watumishi Wake. (Yanibidi niharakishe.) Mungu hutia mafuta watumishi Wake. Unaona? (Sasa, yanilazimu niruke muhtasari mdogo hapa, lakini ningetaka kusema jambo hili.) Hapa . . . Sikiliza sasa, kwa makini, ewe bibi mdogo. Sikiliza kwa makini sasa.

Hapa tunaona mbinu za ibilisi. Tunazionaje? Sasa, ninayo Maandiko mengi sasa hapa, ya manabii na kadhalika, ambapo aliwaendea, na watu mbalimbali katika Biblia aliowafanyia jambo lile lile. Ndivyo ilivyo sikuzote, mbinu zake ni kujaribu kuwafanya watu wasiamini Neno la Mungu.

Sikilizeni, enyi askari wa msalaba! Unapoacha kuamini Neno moja la Biblia ya Mungu iliyoandikwa, umenyang’anywa silaha. Unaamini hilo, Mpenzi? Umenyang’anywa silaha; unajisalimisha. Yavuyavu wee, vaa silaha zote za Mungu! Amina! Tuko vitani. Mungu alichosema ni kweli, kila neno la binadamu ni uongo. Unaona?

Lakini mara tu wewe—anakufanya kusikiliza jambo moja, hizo ndizo mbinu zake, umenyang’anywa silaha. Ni mambo mangapi yaliyompasa Hawa kusikiliza? Moja; alinyang’anywa silaha papo hapo.

Ibilisi alifanya nini? Aliingia ndani moja kwa moja kupitia akili zake hadi kwenye roho yake, na hapo akapotoshwa. Hiyo ni kweli? Alipotoshwa, dakika ile ile alinyang'anywa silaha, hapo alipoacha kuamini Neno la Mungu. Sawa! Hapa tunaona mbinu zake.

Askari jeshi wa Mungu wanaamuriwa kuvaa silaha zote za Mungu. Hiyo ni kweli? Sasa, kama ukitaka kuandika Andiko hilo, linapatikana katika Waefeso 6:10 na 13. Unaona? Tulilisoma muda mchache uliopita; ndilo somo letu. Sawa.

Tazama, vaa silaha zote za Mungu. Hebu (mnao muda wa dakika mbili?) —hebu turudi nyuma hapa dakika moja. Hebu tuone tu silaha zote za Mungu ni nini? Sawa. Tuanzie kwenye aya ya 10. Sasa, sikiliza kwa makini sasa. Hebu tuone silaha zote za Mungu:

Hatimaye, ndugu zangu, . . .

Sasa, najua mimi nakwenda . . . Sasa ni saa sita na dakika ishirini sasa hivi, karibu tu. Mimi—si—sikutaka kuwafundisha muda mrefu leo, bali mimi—huenda mimi nisiwe na ujumbe mwingine zaidi, hadi nitakapofanya baadhi ya ziara zangu kwa msimu wa kiangazi (unaona?) na . . .

Mnajua nini? Mnajua kwa nini ninafanya hili? Nitawaambia. Juzijuzi niliota ndoto. Sikuwa niisimulie, bali iko akilini mwangu; afadhali niiseme.

Baada ya Bwana kunipa tafsiri, niliota kwamba nilikuwa ninajitayarisha kuvuka mto mkubwa kwa kazi ya umishenari. Na mimi . . . Kwanza, nilikuwa juu kule na mke wangu, wangapi waliwahi kumjua George Smith, Smith wa "Sekunde sita," hapa mjini? George Smith, mvulana wake yuko katika jeshi la polisi hapa. Yeye—maskini George sasa ni mlevi kabisa. Bali alikuwa mmoja wa wapiganaji bora sana. Yeye ndiye aliyenipa mazoezi yangu, kabla hata ya kwenda YMCA na po pote. Alikuwa akitufanyiza mazoezi. Naye alikuwa mwepesi, mwepesi sana na akiwa tu mwana ndondi wa uzito wa kati, wa ratili 145, naye alinifundisha mimi. Alikuwa akisimama pale juu; naye angeinua konde lake hivyo, na kunitwanga tumboni, akaniinua akanigandamiza ukutani (unaona?), bali—na isingenisumbua. Alinipa tu mafunzo, hata haikuwa kitu ila mafunzo tu.

Na kisha ni—niliota usiku wa juzijuzi kwamba nilimwona Smith wa "Sekunde sita" (sasa, halikuwa ono, ilikuwa ndoto), na nilimwona Smith wa "Sekunde sita"—vijana wadogo wakija dhidi yake kupigana miereka. Na yeye—yule mzee kama—loo, nadhani, mimi nina umri wa miaka hamsini na miwili; yeye ana kama hamsini na minane, sitini— hakuna mmoja wa hao vijana angeliweza kumgusa kwa njia yo yote. Angewabana pamoja, namna hiyo, akawaangusha chini sakafuni na kuwashikilia kwa mkono wake. Sasa, niliwaza, "Ajabu hiyo," nami nilidhani mke

wangu alikuwa pamoja nami, nami nikasema, "Ajabu hiyo." Nikasema, "Unajua nini, Meda? Alikuwa kocha wangu."

Akasema, "Na—nakumbuka jambo hilo, wewe ukiniambia hilo."

Nikasema, "Ndiyo, bwana! Kwa mafunzo yake mazuri nilishinda mapambano kumi na matano ya kulipwa kisha nikaacha ka—kazi hiyo nipate kuihubiri Injili."

Punde tu ikabadilika, na nilikuwa ninaanza kuvuka ma—maji. Lakini nilipokuwa ninakwenda, nilikuwa nikienda kwa motaboti. Nami nikaangalia kule ng'ambo, na hapo waliketi wawili kati ya ndugu zangu, wameketi mle katika mtumbwi, wakijitayarisha kwenda pamoja nami. Nikasema, "Hamwezi kufanya hivyo, wandugu. A-ha a-ha. Yanibidi kwenda peke yangu."

Kisha yule baharia akaja akasema, "Hii hapa boti yako," mtumbwi mweupe kabisa, wa plastiki.

Nikasema, "La, a-ha a-ha, si huo."

Akasema, "Vema, unaweza kwenda mbio nao upande huu maili hamsini kwa saa."

Nikasema, "Lakini yanibidi kuvuka upande ule." Unaona?

"Vema," akasema, "nenda na hao jamaa."

Nikasema, "Wao si mabaharia. Hawajui ya kutosha kuhusu jambo hilo, wana shauku. Hawawezi kuiendesha hiyo; watakufa maji wote wawili nje huko; hawawezi kabisa!"

Basi akasema, "Wewe ni—unaweza kuamini . . .?"

Nikasema, "Sikiliza, na—najua mengi zaidi kuhusu boti kuliko wanavyojua, na nisingejaribu kuiendesha kwa hicho—kifaa cha namna hiyo." Nikasema, "Inabidi kuchukua motaboti kuivuka hiyo." Nikasema, "Itahitaji kitu fulani kikubwa kuliko huo."

Na nikamwona akiangalia pande zote kwa mmoja wa wale ndugu akasema, "Je! nyinyi ni mabaharia?"

Wale ndugu wakasema, "Ndiyo." Unaona? Nikasema, "Hilo ni kosa."

Na yule baharia akarudi; akasema, "Nitakwambia la kufanya." Kasema, "Wanakupenda; wanakuamini, lakini" kasema, "kama ukijaribu kuvuka kwa motaboti, hao watajaribu kukufuata wewe katika mtumbwi ule; wote wawili watakufa." Unaona? Kasema, "Hawawezi kukufuata."

Nami nikasema, "Vema, nifanyeje?"

Basi huyu baharia bandarini, akasema, "Rudi kule juu." Kasema, "Kuna ghala moja tu ndogo katika nchi hii yote, ghala moja ndogo. Basi weka tu akiba nyingi," kasema, "nao watakaa

hapa. Wata—watakaa hapa, uta—utakapokuwa umeondoka, bali" kasema, "itakubidi kuweka akiba."

Na nilikuwa nikiagiza kila namna ya kabichi, na mboga kama muhogo, na figili, na kadhalika, nikizirundika mle ndani namna hiyo; kisha nikaamka. Sikujua ilikuwa ni nini, bali najua sasa. Unaona? Tunaweka tu akiba, enyi wapendwa. Haya ni maisha ambayo yakubidi kutembea peke yako.

Leo, unakumbuka ile ndoto uliyokuwa nayo wakati ulipokuja hapa mara ya kwanza, kuhusu ile piramidi, na ulifikiri ulikuja mle ndani; nami nilisema, "Leo, hakuna mtu ajaye juu hapa; yambidi Mungu kumweka mtu juu hapa. Ulipanda kila namna ya maumbile ambayo inaweza kupandwa." Nikasema, "Huwezi kuja hapa, Leo. (Unaona?) Shuka urudi kule chini, ukawaambie tu watu kwamba inatoka kwa Mungu. (Unaona? Unaona?) Ni kitu ambacho hu—huwezi ukakitegemea . . . "

Hata ndugu zangu, na dada, na kanisa langu, na kila kitu; na hata makanisa mengine yawe mema jinsi gani, na ndugu zangu kila mahali . . .

Sasa, siwezi kujitenga na kanisa huko nje. Mtu fulani anasema, "Vema, kwa nini unakwenda huko na hao watu, hao watu wa Utatu, wote *hawa, wale* na *wengine,* wale wa Oneness, na Jina la Yesu, na yote haya mambo mengine nje hapa. Kwa nini unachanganyika nao?" Ni wangu. Haidhuru wamefanya nini, wao ni wangu. Wao ni mimbara yangu.

Wakati Israeli walipotenda uovu mbaya sana, mpaka hata Mungu akamwambia Musa "Jitenge; nitaanza kabila—kabila jipya nawe," Musa alijitupa njiani akasema, "Kabla ya Wewe kuwaangamiza, niangamize mimi."

Haidhuru wamefanya nini, hao ndio ambao nimetumwa kwao. Yeye hupeleka Nuru, si iangaze mahali penye Nuru, ni palipo na giza; hapo ndipo mahali pa Nuru. Na yakubidi uchukuane na watu; yakubidi usimame pamoja nao haidhuru nini. Yakubidi . . .

Katika makosa yao . . . Israeli alikuwa amekosea kupindukia. Walikosea sana, hata Mungu akawaacha, bali Musa . . . Sikuzote nimestaajabu jinsi hilo lilivyofanyika, bali Huyo alikuwa Roho wa Kristo katika Musa. Unaona, unaona? Sote tumekosea. Yeye alitupigania sisi sote, tulipokuwa katika makosa yetu.

Haidhuru hao wamekosea jinsi gani, hebu tusijiondoe kwenye ushirika au kujitenga sisi wenyewe na kitu cho chote. Maadamu tunaweza kumvuta mtu, hebu na twende na "busara kama nyoka, wapole kama huwa" (unaona?), na tujaribu kumvuta kila mtu tuwezaye.

Sasa, huku ni, jambo ninalonena asubuhi hii, ni kuhifadhi Chakula, kuhifadhi Chakula, ili kwamba mpate kitu cha kula, ili kwamba mpate kitu cha kufanyia karamu. Kiwekeni Hicho

kwenye kanda zenu; mkaziweke katika chumba chenye baridi. Pengine wakati mrefu baada ya kuondoka kwangu, mngali mtakumbuka mambo haya ni kweli. Ketini chumbani mwenu mkazisikize. Mnaona? Na hiki ni Chakula, kihifadhini Hicho katika ghala. Sijui safari yenyewe ni ya wapi, bali hata iwe ya wapi, Yeye anajua ambako anaongoza; mimi sijui. Ninafuata tu.

Sasa, alisema nini hapa sasa? Sikiliza kwa makini!

> *Hatimaye, ndugu zangu, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake,* (Iweni hodari katika uweza wa nguvu Zake.)
>
> *Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za shetani.*
>
> *Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama;*. . .(kupigana risasi na kukatana kwa visu, mnaona, si jambo hilo). . .*bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa*. . .*giza la dunia hii,*. . . (wakuu wa giza). . .

Nani anayetawala ulimwengu? Ibilisi. Hakika. Ni nani ambaye anaendesha mambo yote haya, mambo yote haya maovu, yanayotendeka mahali pote hapa, na hizi serikali, na kadhalika? Yote ni ibilisi; Biblia ilisema hivyo. Ibilisi hutawala katika Marekani; ibilisi hutawala Ujerumani; ibilisi hutawala kila taifa ulimwenguni. (Ninalijia hilo mnamo dakika chache.) Nasi tutaona iwapo anatawala au la, kama kila ufalme uliowahi kuwepo na utakaowahi kuwepo, mpaka ninino—Mungu atakapoanzisha Ufalme Wake, unatawaliwa na ibilisi. Sasa, sina maana kwamba kila mtu aliyemo mle ni ibilisi. Kuna wacha Mungu mle—katika afisi za serikali.

Atakuja hapa mmoja mnamo siku chache usiku, papa hapa, kuonyesha sinema hapa na Ndugu Arganbright hapa mahali hapa. Amekuwa balozi kwa maraisi watano mbalimbali, Ndugu Rowe, na yeye ni. . .(Atakuwa hapa, nafikiri ni katika juma la pili mwezi wa Aprili. Ndugu Neville atatangaza hilo.) Na yeye ni mtu mzuri sana.

Alisema anaweza kunena katika lugha nane mbalimbali (naamini) lakini alipompokea Roho Mtakatifu, hakuwa na lugha ya kuweza kuzungumza na Bwana; kwa hiyo Bwana akampa moja, alisema, kwa hiyo aliweza kuzungumza Naye kwa hiyo—alimpa mpya ambayo hakufanyia mazoezi. Sawa.

> . . .*juu ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.*
>
> *Kwa sababu hiyo*. . .(Sasa, sikilizeni, enyi askari wote sasa, kabla tu hatujaanza mstari wa maombi.). . .*twaeni* zenu—*twaeni*. . .(z-o-t-e). . .*zote*. . .(siyo sehemu yake tu). . .*silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu,*. . .(Hiyo ni siku tunayoishi.) *na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama.* (Simameni! Amina!

Unalipata hilo? Unaona, Mpenzi, uishapo kuyatimiza yote uwezayo kutenda simama, basi simama, usisogee!)

Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni. . . (Sikiliza hili, sikiliza hili ni nini.). . .*viunoni*. . .(Yaani sehemu yako ya katikati hapa. Unaona?). . .mmejifunga *kweli*. . .(Kweli ni nini? Neno la Mungu. Hiyo ni kweli. "Neno Lako ni Kweli." Basi.). . .*na kuvaa dirii ya haki kifuani,*. . .(Yaani, tenda kilicho haki—una Neno la Mungu ndani yako, ukitenda yaliyo haki.). . .*dirii ya haki;*

Na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani; (Unaenda po pote, mahali po pote, wakati wo wote; miguu imefungiwa Injili. Unaona? Tena angalia!)

Zaidi ya yote. . .(zaidi ya yote hayo). . .itwaeni *ngao ya imani*. . .(Hiyo ndiyo inayoiangusha mishale. Unaona?). . .*ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote ya yule mwovu.*

Tena ipokeeni chapeo ya wokovu,. . .Hiyo ni nafsi, akili—akili humu ndani—kichwa—hukifunika kichwa.). . .na ile*—na upanga wa Roho, ambao ni neno la Mungu:*

Utaifanyiaje chapeo hii, inafanya nini? Ni kinga. Chapeo imetengenezwa kutokana na nini? Shaba nyeupe! Shaba nyeupe haiwezi kutiwa matiko— ni ngumu, ngumu kuliko chuma. Kofia ya shaba nyeupe— nini? Wokovu, ujuzi wa jambo hili: "Kwamba kuponywa kwangu hutoka kwa Mungu; wokovu wangu hutoka kwa Mungu; ujuzi wangu unaambatana na Neno Lake," si wazo la kanisa, Neno. Amina! Ndivyo ilivyo. Kufunikwa kwa kinga. Chapeo ya wokovu, ukombozi, chukua hiyo kisha uendelee mbele kwa kupiga hatua mbele. Loo, sasa! Sasa, hilo ndilo tunalopaswa kutenda.

Jeshi la Shetani, sasa angalia. (Sasa, sisi—yanibidi niharakishe, bali ya—yanibidi niingize hili ndani.) Jeshi la Shetani huleta magonjwa. Hivyo ndivyo alivyo Shetani, yeye ni mharibifu. Shetani—ufalme wote wa Shetani ni maradhi, mauti, na huzuni, na mahangaiko ya moyo, na wasiwasi—vyote juu ya Shetani. Mungu ni Uzima, imani, furaha, amani, huku. Unaona?

Sasa, hizo ndizo zile nguvu kuu mbili zinazopambana sasa hivi. Zinapigana; zinapigana papa hapa katika jengo hili sasa hivi. Zinapigana na wewe siku baada ya siku. Kila nguvu, Shetani akikufuatilia, yule Goliathi mkubwa mno, wa kifalme, na wa kikasisi, akijaribu kukufadhaisha kupita kiasi, yuko. . . Lakini Mungu, umeimarishwa, (Amina!) kwa Injili, kwa Neno la Kweli viunoni mwako. Utukufu! Mhubiri, jambo ndilo hilo: chapeo ya wokovu, ngao ya imani, na Upanga ukitikiswa mkononi mwako. "Shetani, naja kupambana nawe. Unanijia

kwa jina la sayansi; unanijia kwa jina la—la utamaduni; unanijia kwa jina la madhehebu; unanijia kwa jina la *hili, lile,* au *lile jingine;* bali ninakujia katika Jina la Bwana Mungu wa Israeli! Ninakujia. Simile!" Hata kifo chenyewe hakiwezi kusimama pale. Toboa tundu ndani yake. Hilo ni kweli.

Jeshi la Shetani huleta maradhi, na jeshi la Mungu limeagiza kuyaondoa. Amina! Haya basi. Kila wakati Shetani anapokutupia cho chote, jeshi la Mungu lapaswa kumtoa. Amina! Mtoe, hiyo ndiyo mbinu hasa ambayo Mungu alitumia. Shetani alitumia jeshi la uharibifu kwa kutokuamini Neno la Mungu, na kujitengenezea ufalme bora kuliko aliokuwa nao Mikaeli, ndipo Mungu akamtupa nje.

Njia ya Mungu ni kutupilia mbali uovu, kutupilia mbali hoja, kutupilia mbali ushirikina, kutupilia mbali uchovu, kutupilia mbali magonjwa, kutupilia mbali dhambi. Amina! Wewe uko juu yake, umefufuka katika Kristo Yesu ukiketi katika ulimwengu wa roho na kila pepo chini ya miguu yako. Akianza kutokeza kichwa chake hapo, basi . . .

Unajua, umekufa; uhai wako umefichwa. Kitu gani kimekufa? Umekufa kwa hisi zako; umekufa kwa dhamiri zako (mapenzi yako mwenyewe ya kibinadamu yangesema, "Ndiyo, nadhani mimi . . ."), umekufa kwa hoja zako, umekufa kwa mambo yote hayo, nawe umezikwa katika Jina la Yesu Kristo na kufufuliwa pamoja na Yeye. Na po pote alipo Yeye, wewe nawe upo hapo pia.

Kulitukia nini wakati wao—mmoja wa hao wanaoshuku alipofika Mbinguni? Mungu alimtupa nje. Na yeye aliwaambiaje askari waliofufuka katika Kristo? Ibilisi ajapo mpigeni teke! Mtupeni nje!

Wakati Yesu alipofundisha jeshi Lake na kuwatuma hadi miisho ya ulimwengu: "Enendeni ulimwenguni kote, hubirini Injili kwa kila kiumbe. Yeye aaminiye na kubatizwa ataokoka; yeye asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na waaminio, askari Wangu: kwa Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; watashika nyoka; au wakinywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya."

> Twendeni, askari Wakristo,
> Kama katika vita,
> Huku msalaba wa Yesu
> Ukitutangulia! . . .

"Nimesulubiwa pamoja na Yeye; hata hivyo ninaishi; si mimi ninayeishi, bali Yeye anaishi ndani yangu." Neno likitangulia, Mungu akitengeneza njia kwa upanga Wake wenye makali kuwili. Mharibuni.

Si ajabu, wakati Grant alipouteka Richmond, na maskini yule mwanamke mdogo wa kusini akamwona Grant akija, alipata upako akasema:

> Macho yangu yameona utukufu wa kuja
> Kwake Bwana;
> Anakanyaga palipowekwa mavuno ya zabibu
> kwa hasira,
> Aliutoa umeme mwaminifu kwa upanga
> Wake mwepesi na wa kutisha;
> Majeshi Yake yanasonga mbele. Amina!

Grant aliutekaje Richmond? Mara alipofika kule. Amina! Hivyo ndivyo alivyouteka Richmond. Hivyo ndivyo wanajeshi wa Mungu wanavyoshinda dhambi, maradhi— mara wanapoyafikia. Amina! Hivyo ndivyo wanavyoshinda mashaka, na woga, na kadhalika. Mmoja anapoinuka, wao wanamkatilia mbali, kumwondosha njiani. Loo, jamani! Ndivyo ilivyo.

Mungu aliwatoa, kama Yeye alivyofanya Mbinguni. Kapteni wetu Mkuu maarufu alituonyesha jinsi ilivyotendeka.

Roy Roberson, Ndugu Funk, wengi wenu ninyi wanajeshi wa siku nyingi hapa, mwajua kapteni halisi ni nini.

Siku moja nilipokuwa mdogo tu. . . Idara ya Zimamoto ya Jeffersonville chini hapa . . . Nyumba ya Fowle ilishika moto, na hii hapa Idara ya zimamoto ya Jeffersonville wakisimama chini kule, na kapteni akitembea huku na huko akasema, "Rusha maji kidogo kule juu" [Ndugu Branham anaiga sauti ya maji yanayofoka kwenye bomba dogo—Mh.]—kama bomba dogo nje hapa. Hapa kukaja Clarksville, "Rusha maji kidogo hapa." [Ndugu Branham anaigiza sauti ya maji yanayofoka kwenye tundu dogo sana kupitia kwenye bomba la kumwagia maji—Mh.] Jumba la Fowle likateketea.

Wakapiga simu Louisville; huyu hapa anakuja mtu aliyefunzwa. Loo, jinsi hivyo ving'ora vilivyolia kila mahali hapo! Na hawa hapa makapteni wakuu hapa wa idara hizi za zimamoto wanasema, "Rusha maji kidogo juu hapa; rusha maji kidogo chini hapa"— mtu asiyefunzwa. Ndugu, mara tu mtambo ule uliposimama, nani aliyekuwa juu kabisa ya ngazi? Kapteni! Wakati ngazi hiyo ilipopandishwa juu, alikwea pamoja nayo. Ilipogonga dirisha (alikuwa hajafikia kwenye dirisha bado), alikamata shoka lake, na akalitupa kupitia kwenye dirisha, akasema, "Njoni, enyi vijana." Moto ulizimika mnamo dakika chache. Kapteni! Hakuwa kapteni wa kusema, "Rusha maji kidogo hapa; jaribu kidogo hapa," bali, "Njoni, enyi vijana." Amina. Aliongoza njia; alituonyesha jinsi inavyofanywa.

Nikawaza, "Idara hiyo ya zimamoto iliyofunzwa vizuri sana, waliuzima moto ule kwa dakika chache." Kwa nini? Walikuwa na kapteni pale aliyejua alilokuwa anafanya.

Ndugu, nena kuhusu theolojia yako yote unavyotaka kunena, madhehebu yenu yaliyoundwa na binadamu, mashirika yenu. Cheza nayo! Nina Kapteni Mkuu aliyeniambia jinsi ya kulitenda. Wasema, "Naam, kama naweza kusikia harufu yake, kuihisi . . ."

Loo upuzi! Hivi ndivyo yule Kapteni Mkuu alivyosema inafanywa katika Luka sura ya 4. Sina muda wa kuisoma; isome wewe mwenyewe asubuhi hii, Luka sura ya 4 kuanzia kwenye aya ya 1. Hakusema kamwe, "Sasa, nawaambia. Hebu nendeni huku mkaunde madhehebu maarufu; wekeni wazee, na mashemasi, na—au wekeni makadinali na maaskofu na wekeni *hili*." Hakusema hilo kamwe.

Shetani alipokutana na Yeye, alisema, "Sasa, wewe una njaa; geuza mawe haya yawe mkate."

Alisema, "Imeandikwa."

Alisema, "Juu huku, tutakuchukua juu huku na kukuonyesha jambo fulani."

"Lakini Imeandikwa!"

"Nitatenda hili kama uta . . ."

"Imeandikwa!"

Hivyo ndivyo yule Kapteni Mkuu alivyosema linatendwa. Linatendwaje, Dada? Imeandikwa: "Ukiweka mikono yako juu ya wagonjwa watapata afya." Imeandikwa: "Kwa Jina Langu watatoa pepo." Amina! Ni nini? Imeandikwa. Hiyo ndiyo amri ya Kapteni. Imeandikwa: "Yeye ayasikiaye maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka Mimi yuna Uzima wa Milele." Imeandikwa; imeandikwa; imeandikwa; hizo—hizo ndizo amri; huyo ndiye askari; hiyo ndiyo njia; hiyo ndiyo mizinga tunayosogeza mbele.

Alifanya nini? Alikwenda moja kwa moja kule kwa Goliathi. Yeye alituonyesha . . . Daudi alionyeshaje jeshi jinsi ilivyotendeka? Daudi aliwaonyeshaje Israeli jinsi ilivyofanywa? *Daudi* linamaanisha *mpendwa, mwokozi*. Unaona? Daudi alilifanyaje? Alisema, "Hivi ndivyo linavyofanywa: tumaini Neno la Bwana."

Basi Goliathi akatokeza pale, akasema, "Wajuaje? Nitakuokota kwa ncha ya mkuki huu, nitakulisha ndege wewe."

Akasema, "Unanijia kama madhehebu; unanijia kama mwanasayansi wa kisasa; unanijia na upanga wako mkubwa mno wa futi kumi na nne, unanijia na chapeo ya shaba nyeupe na kipande cha ngao ambacho hata siwezi kukiinua toka ardhini; unanijia kama shujaa aliyepata mafunzo; unanijia na Ph.D, na L.L.D na L maradufu D; unanijia na mambo haya yote; bali mimi naja katika Jina la Bwana Mungu wa Israeli, na leo nitakikata kichwa chako toka kwenye mabega yako." Amina!

Maskini kijitu hicho, kikijitokeza pale kulikabili hilo pandikizi la mtu, lakini alijua anakosimama. Israeli wakiwa tu wanatetemeka nyuma kule, "Loo, maskini kijitu kile."

Goliathi akasema, "Nitakuonyesha ambaye nitamtengeneza," na hapa yuaja.

Alikuwa na I-m-a-n-i (unaona?) k-a-t-i-k-a J-e-s-u-s, miamba mitano, mawe matano. Kijiwe kimoja ndani hapo cha kuanzia. Akikizungusha pande zote namna hiyo, Roho Mtakatifu akalishika jiwe hilo nalo likaenda; basi Goliathi akaanguka ardhini. Hivyo ndivyo ifanywavyo.

Hivyo ndivyo Yesu alivyosema Yeye aliposema, "Sasa, kama ninyi ndugu mnaenda uwanjani, kama tunataka kujua jinsi ya kuwashinda hawa pepo, nitawaonyesha namna inavyofanywa."

Shetani akasema, "Nitakabiliana nawe (Goliathi); nitakuonyesha ninachoweza kufanya. Una njaa; ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, nitashindana nawe. Unasema u Mwana wa Mungu; nitashindana nawe. Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, geuza mawe haya yawe mkate. Kula, una njaa. Na kama u Mwana wa Mungu, unao uwezo wa kufanya jambo hilo."

Akasema, "Lakini imeandikwa: 'Mtu hataishi kwa mkate tu.'" Loo, hivyo ndivyo yule Kapteni Mkuu alivyolifanya.

Akamchukua akamweka juu ya kinara cha hekalu akasema, "Kama ukijitupa chini," akasema, "unajua, imeandikwa pia . . . "

Yeye akasema, "Ndiyo! Pia imeandikwa tena: 'Usimjaribu Bwana Mungu wako.'" Unaona Yeye alivyojiita? *Bwana Mungu wako*. "Usimjaribu Bwana Mungu wako." Imeandikwa tena namna hiyo. Unaona?

Loo, jamani! Yeye alifanya nini? Yeye alimshinda kwa Neno la Mungu. Mbinu ya ibilisi ni kukufanya usiamini Neno la Mungu, na Kapteni Mkuu anasema uchukue Neno la Mungu ukatende jambo hilo. "Kwa Jina Langu watatoa pepo."

Loo, Shetani, kapteni wao mkuu, loo, unajua, baadhi ya haya madhehebu yanajaribu kukufanya uamini ana ukwato panda, unajua, na mkia uliogawanyika, na upuzi huo wote. Usiamini jambo hilo. A-ha, a-ha! Hayuko jinsi hiyo. La, bwana, Ndugu; yeye ni mjanja sana. Usiamini ana hayo. Wanafanya tu jambo hilo kusudi wakutie hofu; huyo si ibilisi. Ibilisi kwanza hana ukwato. Nalitilia jambo hilo shaka sana. Yeye ni—yeye ni roho; ibilisi ni roho. Yeye hana kwato panda na vitu hivyo jinsi wanavyojaribu kumwazia. La, la! Bali ni mwerevu. Ndugu, yeye ni mtu mwerevu sana, mtu aliyeelimika kwelikweli (sikuzote imekuwa hivyo) katika hekima ya kidunia. Loo, ndiyo! Yeye ana sura nzuri. Ameliunda jeshi lake kwa hekima ya kidunia, hadi, Ndugu, usijaribu ku—usijaribu kunena maneno yako. Yakupasa

ujue unalolizungumzia unapokabiliana na mmoja wa jamaa hawa wanaosema, “Siku za miujiza zimepita.”

Sasa, yeye hana, hana ukwato panda. Yeye ni—loo, yeye ni—yeye anatoka seminari, ameadibishwa, Ndugu; ninamaanisha ni mwerevu—Ph.D., L.L.D., Q.U.S.D., na zote hizo. Unaona? Loo, ndani mle mwerevu awezavyo kuwa. Mwerevu? Hakika ni mwerevu, yule nyoka—“mjanja” kuliko wote. Nywele zimechanuliwa vilivyo, Ndugu, namaanisha amevaa na hakuna hata kunjo katika koti; mwerevu—ana hekima na ni mwerevu kwelikweli. Hilo ni kweli. Usimchezee, isipokuwa uwe unajua unachozungumzia. Hiyo ni kweli. Loo, lakini tunajua mbinu—mbinu zake za kale. Tunajua anachojaribu kufanya: kutufanya tusiamini Neno la Mungu. Naye hana kwato panda. La, la! la!

Sasa, tunaona kwamba kama hana kwato panda, basi lazima awe ni kitu kingine. Ni mjanja sana; ni mwerevu, ameelimika, mwungwana. Ndugu, ameliweka jeshi lake hivyo . . .

Angalia! Wakati mmoja huko Uswisi (siwezi tu kupata mahali pa kukomea, jamani) kule—kule Uswisi, kukaja lile jeshi la Kijerumani—adui wakija. Mbona, lilionekana kama ukuta wa matofali! Kila mtu amefundishwa, kila mkuki umewekwa hivi, futi nane au kumi mbele. Nao wakawajia maskini Waswisi wachache juu kule. Walikuwa na nini? Walikuwa wana silaha za—na makengee ya miundu yao, fimbo, na mawe. Nao hao hapo wamesimama; wakakabiliana nao. Huko ng’ambo ya kilima kulikuweko makazi yao. Hapa jeshi la Waswisi lilitoka kwenda kupambana nao. Hawakuwa wamewatendea kitu cho chote. Walikuja tu wakaiteka nchi yao.

Kweli mtoto huyu amefanya nini?—ni mtoto mdogo tu. Shetani, huyo ndiye ambaye angechukua uhai wake kama angeweza. Hakika! Huyo hapo kabla ya wakati wake.

Unaona? Waswisi hawakuwa wametenda lo lote. Walikuwa watu wazuri; walikuwa wakijaribu kulinda makazi yao, bali walisimama nje huko kuyalinda. Baada ya muda kidogo akatokea mtu mmoja jina lake Arnold von Winkelried.

Hili hapa jeshi linakuja; wote walikuwa wamezingirwa. Kasema, “Tufanye nini?” Kila mahali, bahari tu za watu, waliofunzwa vizuri. Hivyo ndivyo Shetani afanyavyo. Wamefunzwa vizuri, mkuki wake umeelekezwa mbele tu, kila mtu anapiga hatua kwa utaratibu, moja mbili, moja mbili, wakilikaribia tu hili jeshi dogo. Wali—waliendelea tu kutembea, hilo tu ndilo lililowabidi kutenda huku wakiwaokota, kila mmoja, kwa mapanga yao; ile mikuki ikiwachoma moja kwa moja miilini mwao. Huo ungekuwa ndio mwisho wa jeshi la Kiswisi; hamna jambo lingine.

Huko juu kilimani kulikuwa na makazi yao pamoja na wapenzi wao. Na hao wanawake wametendwa jeuri, na kunajisiwa, na binti zao wadogo na watoto wameuawa

na nyumba zao zikachomwa moto, na kila kitu, chakula kimechukuliwa, mifugo na kadhalika vimechukuliwa. Hao hapo. Kulitukia nini?

Uvuvio ulimwingia mtu mmoja jina lake Arnold von Winkelried. Akasema, "Enyi watu wa Uswisi, leo hii nitakufa kwa ajili ya Uswisi!" Amina! "Leo hii nitakufa kwa ajili ya Uswisi!"

Wakasema, "Utafanya nini?"

Akasema, "Nifuateni mimi mkapigane na yote mliyo nayo!" Akasimama juu kule, akatupa mkuki wake chini (fimbo yake ndogo aliyokuwa nayo mkononi mwake hivyo); naye akapiga kelele huku ameinua mikono yake, juu hivyo, na akakimbia kulielekea, akipiga ukelele, "Simile uhuru uingie!" Katimua mbio haraka alivyoweza moja kwa moja kwenye lile jeshi, naye alipofanya hivyo, akanyakua kila mmoja wa mikuki aliyoweza na kuichomeka moja kwa moja katika kifua chake namna hiyo, akafa.

Aliwaambia kabla ya jambo hilo, kasema, "Kuna maskini nyumba moja ndogo juu kule, mke, na watoto wachanga wachache." Akasema, "Ninaacha makazi madogo ndiyo kwanza niyanunue." Kisha akasema, "Ni—ninawapenda, lakini leo, nitakufa kwa ajili ya Uswisi." Alitoa—alisema, "Natoa uhai wangu kuliokoa taifa hili." Na huyo alikwa shujaa ambaye... Hawajapigana vita tangu zamani hizo; hilo—hilo liliimaliza. Liliangamiza kabisa jeshi lile, kwa ushujaa ule ulioonyeshwa, mpaka hapakuwa na—lile—lile—lile jeshi lilichanganyikiwa sana, Waswisi waliwavingirishia mawe, na kuwafukuza kutoka nchini, na kamwe hawajarudi tangu wakati huo. Hayo yalikuwa mamia ya miaka iliyopita. Unaona? Kwa nini?

Hilo lilikuwa tendo kubwa, bali loo, Ndugu, siku moja wakati ujinga, ushirikina, shaka, kuhangaika, na woga viliwagandamiza watu wa Mungu pembeni, kulikuwa na Mtu mmoja jina Lake Yesu Kristo aliyesema, "Leo hii nitakufa kwa ajili ya watu." Hiyo ni kweli.

Aliliambia nini jeshi Lake? "Nifuateni Mimi mkapigane na kila kitu mlicho nacho. Kama una rungu, shambulia kwa rungu; usiogope! Kama una fimbo, shambulia kwa fimbo. Kama una jiwe, shambulia kwa jiwe, cho chote ulicho nacho!" Hivyo ndivyo Kapteni wetu Mkuu anavyosema leo. "Nimelichukua Neno la Mungu na kumshinda ibilisi katika nguvu zake." Alimkatakata vipandevipande (Amina) kwa lile Neno.

Sasa lo lote ulilo nalo, kama unalo Neno moja tu, "Bwana Mungu Mungu wako, ndiye akuponyaye." Mkatekate! Mfuate Yeye (Amina!), mfuate Kapteni wetu. Ndiyo, bwana, Yeye alimkata.

Shetani na milki zake kubwa na nzuri, na uzuri zaidi, na kila kitu, vyote vya kisasa havituhusu sisi. Hilo ni kweli. Yeye yungali

mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu. Ndiyo, bwana! Yesu alisema kwamba wana wa ulimwengu huu wana busara kuliko wana wa Ufalme wa Mungu.

Sasa, haya mapambano mawili makuu (tuta. . .yanibidi—yanibidi kufunga), mapambano haya mawili yanakabiliana sasa hivi. Hivi sasa ndiyo saa ambapo magonjwa na kadhalika vimeukumba ulimwengu, mpaka sayansi ya utabibu imeduwaa, na kila kitu kimeduwaa; hakuna kitu. . .Sisi tu. . .Nalo jeshi, jeshi dogo la Mungu limegandamizwa pembeni na kila kitu. Ndugu, wakati wa Arnold von Winkelfried mwingine umewadia.

Wakati umewadia, wakati wa mtu mwingine wa Mungu kusimama mbele; wakati wa kutokea kwa Eliya umewadia. Wakati umewadia wa jambo fulani kutukia; Jeshi la Mungu, fungeni akili zenu; msisimame kwa dakika moja kuwaza juu ya cho chote anachokupa ibilisi kupitia hisi zako. Bali kumbuka, Neno la Mungu haliwezi kushindwa kamwe. Majeshi haya makuu mawili. . .

Adui ajapo kama mafuriko, kama anavyokuja leo, Mungu alisema Yeye angefanya nini? Roho wa Mungu atainua beramu dhidi yake. Je! wewe ni mmoja wao? Ndiyo, bwana!

Tunafundishwa katika Yakobo 4:7 (sina muda wa kulisoma), Yakobo 4:7, kumpinga ibilisi, naye *hatatembea tu akienda zake*, bali atakimbia. Mpingeni ibilisi! Unampingaje ibilisi? Namna ile Kapteni wetu Mkuu alivyotuambia kufanya jambo hilo. Chukua Neno la Mungu; hivyo ndivyo unavyompinga ibilisi ni kwa Neno la Mungu. Kapteni Mkuu alituambia namna tu ilivyotendwa. Sawa.

Sasa katika kufunga, nataka kusema jambo hili: yule ibilisi wa kale, sasa mnadhani ana haya; mnadhani atamshambulia mtoto? Atashambulia cho chote; alimshambulia Yesu Kristo. Alimjia na mashambulio matatu makali. Ulijua jambo hilo? Shetani hakushambulia tu mara moja. Atakushambulia kwa ugonjwa, halafu hapa atarudi akushambulie akisema, "Siku za miujiza zimepita. Hukuponywa; hakuna kitu kama hicho." Unajua jambo hilo ni kweli?

Alimshambulia Yesu mara tatu. Alimshambulia Yesu mashambulio matatu makali ya kutokuamini kwake Neno la Mungu. Yesu alikuwa Neno. Hakika, yeye hakuliamini Hilo. "Ikiwa wewe ni. Ikiwa wewe ni!" Huyu hapa anakuja, mashambulio makali, kama wakati mwingine adui anavyofanya. Huyu hapa anakuja, kasema, "Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu nionyeshe muujiza; hebu nione ukifanywa." Ndugu, mashambulio matatu makali aliyoingia nayo, "Ikiwa wewe—ikiwa wewe ni."

Sasa, Yesu alifanya nini? Yesu alikuwa Neno la Mungu; Yeye alikuwa Neno. Alishambulia Neno. Utukufu! Ni—ni—ninaanza tu kujisikia vyema kuhubiri sasa, kweli najisikia

hivyo. Yesu ni Neno. *Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.* Naye Neno akakaa—alifanyika mwili akakaa . . . Yesu alikuwa Neno. Alifanya nini? Yeye alimkatakata vipandevipande. Loo, jamani! (Nitamaliza.) Yesu alifanya nini? Yeye alikuwa Neno, kwa hiyo kwa Neno alimkata Shetani kwenye mashambulio yake makali. Alimrukia pale kama kikosi cha—kikosi cha askari hodari wanoshambulia ghafla au kitu kama hicho, alimrukia Yesu, lile Neno, namna hiyo, Naye Yesu akalichukua hilo Neno na kumkatakata vipandevipande. Haleluya. Hakika, alimkata vipandevipande, akamshinda kwa Neno.

Unaona shambulio lake? Angalia! Sikiliza kwa makini ninapofunga. Shambulio lake ni nini? Kutokuamini Neno la Mungu, hilo ndilo shambulio lake. Hapo, unaweza kuona vita vikuu sana vilivyopata kupiganwa? Kuna nguvu mbili tu: Shetani na Mungu. Na silaha ya shetani dhidi yako ni nini? Ni kujaribu kukufanya usiamini Silaha yako. Anakunyang'anya silaha. Hebu—hebu tusikilize kwa makini sana sasa, sikilizeni.

Kama anaweza kukufanya usiamini Silaha yako ni sawa, akikufanya kuamini kwamba Silaha yako haina nguvu vya kutosha, amekunyang'anya silaha. Loo, Ndugu Neville, natumaini hutaacha kamwe kuamini jambo hilo! Bali, anakunyang'anya silaha, anapokufanya usiamini Silaha ile. Unapoweka Hiyo chini, mapambano yako yamekwisha; umeshindwa. Shikilia Silaha ile; usiiweke Hiyo chini! Tunaona kutokuamini kwake. Hebu . . . Nataka kusema jambo moja zaidi sasa punde kidogo.

Urusi . . . Nitasema jambo hili kwa ajili ya hawa mashujaa, na kadhalika, na ninyi wanafunzi wa Biblia. Mnafanya fujo na kupiga makelele ya nini kuhusu Urusi? Hamnisikii mimi nikiwaambia mjenge ngome za kujikinga na makombora, sivyo? Mbona hizi fujo kuhusu Urusi? Urusi si kitu; hawatashinda vita vyo vyote; hawatautwaa ulimwengu wo wote. Ukomunisti hautauteka ulimwengu wo wote. Hivi watu wana nini? Neno la Mungu linaweza kushindwa?

Sikilizeni, liko kwenye kanda sasa. Ninauzungumzia ulimwengu au po pote kanda hizi zitakapokwenda. Na kwenu ninyi watu hapa, haidhuru nini kitakachonipata, ninyi aminini jambo hili. Urusi, ukomunisti hauteki cho chote! Neno la Mungu haliwezi kushindwa. Urumi utauteka ulimwengu.

Hebu na tuchukue ono la Danieli; hilo ni Neno la Mungu. "Wewe, ee Daniel—au ewe, ee Mfalme Nebukadreza ni hiki kichwa cha dhahabu—Babeli. Ufalme mwingine utakufuatia, ambao ni fedha (unaona?), ambao ni wa Wamedi na Waajemi; mwingine ni Uyunani, Alexander Mkuu; mwingine utazuka huko Rumi"—na hapakuwa na cho chote kilichosemwa kuhusu u—ukomunisti! Rumi iliuteka ulimwengu.

Yesu Kristo alizaliwa katika ufalme wa Kirumi na kuteswa, mara Yake ya kwanza kuja hapa, na ufalme wa Kirumi. Na katika kuja Kwake mara ya pili sasa, Ujumbe Wake unateswa na madhehebu ya Kirumi, ambayo ni mama wa yote. Na Yeye atakaporudi, atarudi kuuangamiza ule ufalme wa Kirumi, ambapo Wayahudi sikuzote wamemtazamia Yeye kuja na kuuangamiza ufalme wa Kirumi. Utawala wa Kikatoliki na madhehebu yote duniani, sasa hivi yanakusanyika pamoja kama shirika, muungano wa makanisa ukiunda shirika. Si Urusi, ni Rumi! BWANA ASEMA HIVI.

Nionyeshe Andiko moja ambapo ukomunisti au cho chote kile mbali na Rumi kitatawala. Je! Wamedi na Waajemi walimfuata Nebukadreza? Hakika. Je! Uyunani uliwafuata? Ndiyo! Je! Rumi iliutwaa tokea hapo? Je! ilivunjika katika milki kumi za Kituruki kama tu tulizo nazo leo? Je! Eisenhower, ambalo humaanisha *chuma,* Khrushchev humaanisha *udongo,* je! hawakufanya mkutano wao papa hapa kisha Khrushchev akavua kiatu chake kulifanya jambo dhahiri, wazi sana; akapigapiga nacho dawati namna hiyo [Ndugu Branham anapigapiga kwa nguvu mimbara kutoa mfano—Mh.] kuwaonyesha watu? Naam, watu wana nini leo?

Imani imekwenda wapi? Kwa nini—je! humuamini Neno la Mungu ni Kweli?. . .?. . .Kuna matatizo gani kwa wahubiri leo? Ukomunisti, kila mhubiri nje hapa anajaribu kuushambulia ukomunisti. Ukomunisti si kitu! Kitu hicho, ibilisi anakipenyeza moja kwa moja chini ya mapua yenu nanyi humjui. Ni Urumi, umadhehebu, na Rumi ndiye mama wa umadhehebu. Biblia ilisema alikuwa kahaba mkuu na binti zake walikuwa makahaba dhidi ya Mungu, dhidi ya Neno Lake. Enyi askari, litwaeni Neno; . . .?. . .dumuni na hilo Neno!

Nitakufa siku moja, bali Neno haliwezi kufa. Na ninyi vijana, kama hilo halitukii katika kizazi changu, mtaona. Jambo ndilo hilo.

Mmesikia taarifa ya habari asubuhi hii, Mke wa Kennedy akienda kumwona papa, naye papa alisemaje? Unaona? Dini zote za ulimwengu? Loo. Vema, labda tutapata mengine zaidi Jumapili ijayo.

Unaona? Usiwe na wasiwasi kuhusu Urusi. Urusi ni changarawe moja ndogo ufukoni. Usiwe na wasiwasi kuhusu ukomunisti; wewe angalia Urumi, wakati unapounganika na makanisa. Hakuna neno lililoandikwa katika Maandiko kuhusu ukomunisti kutawala ulimwengu. Nami huongozwa na Neno, haijalishi kinachoendelea, Neno Ndilo ninaloamini.

Ni Urumi ambao utauteka ulimwengu, na Urumi ni mama wa madhehebu. Hakujawa kamwe na madhehebu yo yote mpaka Rumi, na kila moja yao yalitoka kwake, na Biblia ilisema hivyo.

Yeye alikuwa mama wa makahaba! (Ningeweza kukaa nusu siku kwenye hilo tena, bali nadhani afadhali niendelee.)

Adui anapotushambulia, basi... "Loo, nakwambia, yakupasa uje ujiunge na yetu..." Utafanya nini? Utakubali? Utapatana? Si askari halisi hata. La, bwana! Tunafanya nini basi? Nia, ruhusu nia ile iliyokuwamo ndani ya Kristo...Je! hivyo ndivyo Biblia imesema? Nia iliyokuwamo ndani ya Kristo iwe ndani yenu. Alikuwa na nia gani Yeye? Alidumu katika Neno, Hilo ni sawa! Alidumu katika Neno, Neno la Baba, ndipo akamshinda adui kila wakati.

Sasa, wakati adui anashambulia na kujaribu kusema yakupasa kutenda *hili* na kufanya *lile,* utafanyaje? Dumu katika Neno. Hiyo ni kweli! Utafanyaje basi? Chukua Neno! Neno ni nini? Biblia ilisema hapa, ndiyo kwanza tuisome. Kwa maana Roho ni—wa Mungu ni Neno. Unaona? Angalia hapa. "Tena ipokee chapeo ya wokovu, na Upanga, Upanga wa Roho"—Upanga wa Roho. Ni Roho gani ambayo huja kupitia akilini mwako, na kuingia ndani yako; na Upanga wa huyo Roho ni Neno la Mungu! Huyo Roho anapigana na nini? Roho Mtakatifu anapigana na nini? Kuhisi? Kujisikia?— Neno! Utukufu! Utukufu!

Anapigana akitumia nini? Kuhisi, Neno! Neno! Hebu na tuliseme, Neno! Neno! [Kusanyiko linajibu, "Neno"—Mh.] Neno la Mungu ndilo Roho hupigana kwalo.

Roho wa Mungu huenda moja kwa moja kwa ibilisi na kusema, "Imeandikwa!" Amina! "Imeandikwa!" ndipo ibilisi anaondoka.

Tunafanyaje? Kuchukua Upanga, ambao ni Neno la Mungu, tunauchomoa Huo kwa kutumia nini? Mkono wa imani, mkono wenye nguvu wa imani, Upanga ukatao kuwili. Biblia ilisema katika Waebrania 4, Ni—Ni Upanga ukatao kuwili, hukata pande zote mbili ukija na ukienda.

Ndugu, anafanya nini? Chukua Neno...Chukua Roho, mruhusu Roho aje moyoni mwako, fungua akili yako, useme, "Neno Lako ni Kweli." (Nawe utende hili, Dada.) "Neno Lako ni Kweli. Bwana, sitajali jinsi ninavyojisikia, jambo mtu mwingine asemalo; ninafunga, ninasafisha kila moja ya njia zangu. Mahangaiko yote, na mashaka, na kutokuamini ambako nimepata kuwa nako; kila kuhisi ulikowahi kuwa nako; maradhi yote niliyowahi kuwa nayo; kila kitu kingine nilichopata kuwa nacho; ninavitupilia vyote nje; ninavipuuza vyote na kuja moja kwa moja kwa Roho yangu. Ee Bwana, shuka; Wewe ulisema, Wewe ulinifanya mimi mtu mwenye hiari."

"Ndivyo ulivyo, Mwanangu."

"Sawa, ninafungua moyo wangu na akili yangu. Karibu, Bwana Yesu"; na uinyakue ile imani, Upanga wa Roho, BWANA

ASEMA HIVI! Piga kelele, Haleluya! Amina! Kisha katilia mbali kila adui aliye mbele yako. Jambo ndilo hilo.

Kata kila adui. Iwapo pe—pepo mchafu wa kale anakufanya ujisikie . . . Katilia mbali kitu hicho kwa Neno la Bwana. Nguvu yetu ni, furaha ya Bwana ndiyo nguvu yangu. Ondoka kwangu! Mpige dharuba kisha umkate kwa Neno.

Iwe ni pepo; iwe ni adui; iwe ni maradhi; iwe ni ugonjwa; cho chote kile; chukua hilo Neno ulivute kwa Upanga: na kama—kama ukilipiga dharuba mara ya kwanza nalo halielekei kusogea, lipige dharuba tena, na ulipige dharuba tena, na ulipige dharuba tena! Na ulipige dharuba mpaka umetoboa tundu, kama kifaranga mdogo akijitokeza mwenyewe nje —au tai, ndivyo ulivyo. Jitokeze moja kwa moja kutoka hilo gamba la kale la maradhi, fyeka upate njia ya kutokea, kisha useme, "Haleluya, yuko wapi mwingine?" Amina! Hivyo ndivyo vita; huyo ndiye askari. Huyo ndiye askari wa msalaba. Ndiyo, bwana!

Mtupilie nje kila adui. Kwa nini? Kwa nini? Sisi ni Mzao wa Kifalme wa Ibrahimu uliochaguliwa tangu awali. Wakati Ibrahimu alipokana kila kitu ambacho kilikuwa kinyume cha Neno la Mungu, alikatakata akatupilia mbali kila kizuizi kilichokuja mbele yake. Walisema, "Mkeo ni mzee mno." Alikikatilia mbali kitu hicho.

Ibilisi alisema, "Huwezi kutenda jambo *hili,* na huwezi kutenda *lile.*"

Ibrahimu alikikata akakitupilia mbali. Alikipiga dharuba, akakipiga dharuba, mpaka akajitoa. "Ni wapi tena, Bwana?"

"Peleka hema lako juu hapa." Akaenda naye akajijengea madhabahu juu kule.

Akafika juu kule na Shetani akaja, akasema, "Sasa, nakwambia, hapa si mahali panapofaa."

"Nitakaa papa hapa; ondoka kwenye ardhi yangu!" Haleluya!

Lutu akasema, "Afadhali ushuke uje huku; tuna wakati mzuri chini hapa. Sote tuna shirika huku. Naam, mke wangu ni mkubwa wa shirika la waandishi na kadhalika humu mjini. Nakwambia, yakubidi ushuke uje humu."

Sara akasema, "Ibrahimu . . . "

"Funga mdomo, Sara! (Haleluya!) Tasimama papa hapa! Hapa ndipo Mungu aliponiweka; papa hapa ndipo nitakaposimama. Hapa ndipo Mungu aliponiweka."

Nyote lisifuni jina la Yesu!
Malaika wote na wamsujudu;
Ileteni taji ya kifalme,

Kwake Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama;
Ardhi nyingine yote ni mchanga udidimiao,
Ardhi nyingine yote ni mchanga udidimiao.

Hata kifo chenyewe, kila kitu kingine ni mchanga udidimiao. "Kwake Kristo, Mwamba wenye imara, ninasimama . . . " Mzao wa Kifalme wa Ibrahimu, Mzao wa Kifalme.

Naam, jeshi la Uingereza lililochaguliwa vizuri sana ni jamii ya kifalme ya Uingereza, damu ya kifalme, kila kitu. Na Mzao wa Kifalme wa Kristo ni Kanisa lililojazwa Roho Mtakatifu, lililojazwa na Roho Mtakatifu. Nini? Mzao wa Kifalme kwa ile ahadi, si kwa hisi, bali kwa ahadi ya Mungu. Husimama kwa Neno la Mungu na kufyeka hata wakapata njia ya kupita, wakipiga yowe, "Haleluya!" Hata mauti huja na kusema, "Inakunyemelea kifichifichi."

Sema, "Simile, Yordani, ninavuka." Fyeka upate njia ya kuingilia Nchi ya Ahadi. Amina!

Kunatukia nini? Wakati vita vimekwisha (ninafunga sasa, hakika kabisa), wakati vita vimekwisha, na watakatifu wanapiga hatua taratibu wakija nyumbani . . . Nataka kuwaulizeni jambo fulani. Kulitukia nini—kulitukia nini wakati Hitler alipoingia Ufaransa? Mbona, walisema hata usingeweza kuona mbingu kwa ajili ya ndege zote. Wajerumani walipiga hatua kikakamavu kabisa (unaona?) akisimama tu—wakipita karibu naye, wakisherehekea ushindi.

Stalin alipokuja Urusi, kwa maili nyingi kule nyuma, kila kifaru nyuma kidogo tu ya kingine, aliushambulia tu Berlin kwa mizinga hata hamna kilichosalia. Hivyo tu. Na walipokwenda na hawa Wajerumani—hawa askari wa Kirusi wakisherehekea, waliingia ndani na hilo, unajua, jambo hilo dogo la kuchekesha wanalofanya. Nililiona katika sinema wakati mmoja huko London, jinsi walivyokuja (sinema yenyewe ya jambo ambapo—lililotukia)—waliingia wakisherehekea. Loo, jamani! Tuliposikia kwamba vita vimekwisha, tulipiga yowe, tulipiga filimbi. Wakati hao mashujaa waliporudi, tuliwalaki juu kule; walipiga kelele na kufanya vifijo.

Nilikuwa na binamu, alikuwa kule, kasema aliporudi, wote wa zamani—wale mashujaa wa zamani walikuwa wamejaa majeraha sana hata hawangeweza kutoka kitandani; kwa hiyo waliwavingirisha tu juu ya meli walipoingia, ili kuona ile Sanamu ya Uhuru imesimama. Kasema, "Hao watu wakubwa, wakisimama pale, wanalia tu na kuanguka, namna hiyo, walipoona ile Sanamu ya Uhuru." Wameodoka nyumbani miaka minne wakipigana, wametiwa kihoro na vita na kadhalika, lakini walijua kwamba mke, na mpenzi wa moyo, na mama, na baba, na watoto, na yote waliyopenda yako nyuma ya ile Sanamu ya Uhuru; iliwakilisha walichokuwa wakipigania. Loo,

filimbi zililia, na New York ikaingia kwenye vigelegele, hivyo tu, wakati mashujaa wao walikuja wanapiga hatua za taratibu. Hilo litakuwa ni jambo dogo!

Siku moja wakati Kaisari, baada ya vita vikubwa, yeye alisema, "Nataka shujaa wangu maarufu sana apande gari pamoja nami katika sherehe hii kuu ya ushindi juu ya adui wetu." Na kila mmoja wa maofisa alitengeneza mapambo yao ya manyoya, na wakang'arisha ngao zao, na wakapita taratibu (unajua, namna hiyo) kama—kama askari halisi namna hiyo. Baada ya muda kidogo, maskini jamaa mmoja akaja, amekatwa? Jamani, aliangalia tu juu kwa namna fulani naye akaanza namna hiyo. Kaisari akasema, "Ngoja kidogo, hebu kidogo! Wewe (hata hakuwa amevalia kama a—afisa.)" kasema, "njoo hapa." Kasema, "Ulipata kovu hizo wapi?"

Akasema, "Huko kwenye uwanja wa vita."

Kasema, "Panda juu hapa; wewe ndiye mtu ninayetaka aketi karibu nami." Kwa nini? Alionyesha kwamba alikuwa vitani.

Loo, Mungu amrehemu mtu anayeweza kukata mkono wake kwenye kopo la samaki wa sadini na apate kupewa hongera. Nataka nipate makovu ya vita! Kama alivyosema Paulo, "Ninachukua mwilini mwangu chapa za Yesu Kristo." Hiyo ndiyo sababu ninataka kupigana uwanjani.

Siku moja, wakati Kapteni wetu Mkuu atakapokuja, Ambaye alituvalisha silaha, aliyetupa silaha za Mungu, Roho Mtakatifu akatupa Neno Lake la kupigania, kusimama nje huko; wakati Kapteni wetu Mkuu atakapokuja, nataka kupanda kwenye gari niende nyumbani pamoja Naye; na wewe je? Basi, nimshikapo maskini mke wangu mkono, ninaangalia hapa na kuwaona ndugu zangu, na wake zao, na watoto wao; tutakapoanza kutembea tukishuka zile paradiso za Mungu, na Malaika wakiijaza hewa kwa nyimbo juu namna hiyo; nena kuhusu kusherehekea!

Na vita vitakapokwisha tutavaa taji. Loo, jamani! Loo, askari wa msalaba, asubuhi hii, vuta mkono ule wa imani nje huku na ushike Silaha hii.

Vipi kuhusu hilo, Dada? Uko tayari? Vuta Silaha ile, useme, "Mungu, sijali ambalo—ambalo ibilisi ameniambia, kiasi gani mtu mwingine amenena, asubuhi hii ninaamini. Ninaamini."

Kama nilivyosema juzijuzi, kidogo—naamini Jumapili chache zilizopita, kuna mtu aliyeota ndoto. Aliota kwamba ibilisi alikuwa maskini kitu kidogo cha kale, ndipo akamkimbilia akasema, "Buu!" Naye akaruka nyuma kisha ibilisi akaanza kuwa mkubwa zaidi. "Buu!" Naye akaruka nyuma kisha huyo ibilisi akawa mkubwa na mkubwa. Hatimaye ibilisi akawa mkubwa kama yeye na angemshinda. Alijua ilimbidi ampige kwa kitu fulani, kwa hiyo akaangalia huku

na huko; hangepata cho chote cha kumpiga nacho; akaokota tu Biblia, na ibilisi akasema, "Buu!"

Naye akasema, "Buu!" kwake moja kwa moja, ndipo ibilisi akaanza kuwa mdogo zaidi, na mdogo zaidi, na mdogo zaidi, na hatimaye akampiga akamuua kwa Neno.

Wewe u askari sivyo, Dada? Chukua Neno hilo ukaseme, "Imeandikwa. (Amina!) Sitakufa; nitaishi. Nitaketi kwenye maskani na kumsifu Mungu kwa wema Wake pamoja na watu wengine." Mnaamini hilo, enyi watakatifu? [Kusanyiko linajibu "Ndiyo"—Mh.] Amina! Hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

Ee, Bwana Mungu, Muumba mbingu na nchi, na ijulikane leo kwamba Wewe bado u Mungu. Haijalishi kiasi gani ningehubiri, mambo mangapi ningesema, Bwana, Neno moja toka Kwako latosha.

Leso hizi zimewekwa hapa, zikiwakilisha watu wagonjwa. Ninaomba, Baba wa mbinguni, kwamba baraka Zako na uweza Wako utakaa juu ya kila mmoja wao, nikiweka mikono yangu juu yao. Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba kwamba Wewe utatia mafuta vitambaa hivi kwa Uwepo Wako mtakatifu; kwani imeandikwa katika Neno, si jambo lo lote dhidi ya Neno, bali ilisema katika Neno kwamba walichukua kutoka kwenye mwili wa Paulo vitambaa na aproni; pepo wachafu waliwatoka watu, nao wakaponywa magonjwa mbalimbali.

Sasa, sisi si Mt. Paulo, bali Wewe bado u Mungu, na bado Wewe u Roho Mtakatifu yeye yule. Naweka mikono yangu juu ya leso hizi katika Jina la Bwana Yesu, na kuomba kwamba Wewe utambariki na kumponya kila mmoja wao.

Ee Mungu, huyu anayelala hapa kwenye kitanda, ambaye amekuwa hapa, ni mtoto tu, maskini msichana mdogo mzuri. Hawezi kuishi, Bwana. Shetani amemtendea mabaya, na wapendwa matabibu wa dunia hii wamejaribu sana, bila shaka, kumwokoa mtoto huyu; hawawezi kulitenda. Wamefikia mwisho wa hekima zao; hawajui jambo lingine la kufanya. Bali, Bwana, nina furaha sana kwamba kuna sura nyingine imeandikwa. Tunaweza kufungua ukurasa mwingine, na katika ukurasa huu tunaona Tabibu Mkuu akiingia. Tunamwita Yeye apate kutushauri asubuhi hii.

Sasa, Bwana, je! haikuandikwa hapa katika Neno Lako, kwamba "ishara hizi zitafuatana na hao wanaoamini"? Bwana, iwapo mimi si mwamini, nifanye mwamini sasa. Iwapo huyu msichana mdogo si mwamini, mfanye mwamini sasa. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Pia imeandikwa: "Kwa Jina Langu watatoa pepo." Bwana, hayo—hayo ni maneno Yako; ni Yako, Hilo—Hilo ni Neno Lako.

Na sasa, kama mtumishi Wako, kama Wewe ulivyosema, "Wakiwapo wawili au watatu kati yenu wamekutanika pamoja,

nitakuwa miongoni mwenu; na kama mtapatana, katika kitu kimoja, na kuomba, mtakipokea."

Mungu, mtoto huyu labda ndiye mtu aliye mgonjwa sana katika jengo hili asubuhi hii, kwa sababu hawezi kuishi bila Wewe muda mrefu zaidi, naye ndiye aliye mgonjwa zaidi ya wote. Kwa hiyo sisi sote, tunakubaliana, kama kila askari anayesimama hapa, na katika kundi hili unasimama Mzao wa Kifalme wa Ibrahimu. Tunasogea kumkabili Shetani sasa. Afadhali ujitayarishe kwenda, Shetani, sababu silaha zetu zinametameta, bendera zinapepea, wanaume na wanawake wanashika mapanga, wakipiga hatua mbele sasa kupambana nawe kwa ajili ya msichana huyu mdogo. Toka ndani yake, Shetani! Mwache mtoto huyo! Sisi tukiwa Jeshi la Mungu aliye hai, tunakukataa! Mwache katika Jina la Yesu Kristo! Naenda kumwekea mikono.

Sasa, Shetani, umemfunga mtoto huyu; umefanya uovu huu. Najua kwamba una nguvu zaidi ya binadamu, bali si kitu kwa Bwana wangu, kwa hiyo naja katika Jina Lake. Mwache, wewe roho wa ibilisi. Wewe pepo wa maradhi, toka ndani ya mtoto huyu, na hebu na awe huru tangu leo. Nitalitamka hili katika Jina la Yesu Kristo.

Sasa, Bwana Mungu, Wewe Ambaye ulifufua wafu na kuthibitisha kwamba Wewe ni Mungu, mpe afya huyu kijana mwanamke na nguvu zake tena, ili asimame katika jengo hili hapa. Ibilisi amemtoka. Wewe Ndiwe ambaye unaweza kumfanya mzima. Mjalie aishi kwa utukufu na heshima ya Mungu. I—imekwisha nenwa, sasa na itendeke!

Kuna wengine ndani hapa ambao mnataka kuinua mikono yenu na kusema, "Nataka kuombewa. Mimi ni mgonjwa; namhitaji Mungu." Sijui tuna muda gani. Tuna muda wa kutosha kuwaruhusu hao watu kupitia hapa. Najisikia mwenye ujasiri hasa asubuhi hii. Nataka ushuke uje hapa, Billy, na uchukue tu, labda sehemu hii moja papa hapa, upande huu huku pekee. Hebu upande huu uje kwanza, halafu tutachukua upande wa nyuma baadaye, hadi kwenye marefu yale pale. Halafu tutawachukua hivyo, ndipo hawata . . .

Na sasa nataka Ndugu Neville na baadhi ya ndugu zangu wahudumu kusimama hapa karibu nami, papa hapa, ili muweze kuwarudisha kwenye yale marefu tena. Sawa.

Sawa. Sasa, mimi . . . Wangapi wenu mmevaa silaha zenu? Yuko tofauti sasa; nenda nyumbani upate afya. Amina! Loo, jamani!

Loo, ninyi askari wa vita, chomoeni Upanga, chomoeni Upanga, enyi askari wa msalaba. Mkipiga hatua taratibu, mkipiga hatua taratibu!

Kwake Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama;
Ardhi nyingine yote ni mchanga udidimiao.

Sawa! Njoni, moja kwa moja upande wa jukwaa. Kila mtu katika maombi sasa, huku wakipita. Chomoeni Upanga wenu sasa (Unaona?), endeleeni kupita, endeleeni kupaza sauti. [Watu wanapita kwenye mstari wa maombi—Mh.]

Twendeni askari Wakristo
. . . Kama katika vita,
Huku msalaba wa Yesu
Ukitutangulia!

Simile, Shetani! Kuna nini, enyi askari? Hamfikiri tunaweza kushinda? Tumeshinda tayari. Tu zaidi ya washindi katika Kristo Yesu. Kila pepo ametolewa nje, kila kitu kingine. [Ndugu Branham anaendelea kuwaombea wagonjwa—Mh.]

Nataka maskini bibi yule. . . Huyu mhubiri mdogo ana kasoro hapa. Njoo hapa! Mtu huyu alipelekwa nyumbani kutoka hospitalini juzijuzi, akifa, ameliwa na kansa, mwaka uliopita—miaka miwili iliyopita akiwa na ugonjwa wa kuvunjika nguvu. Ndiyo—madaktari walimpa tu siku chache za kuishi. Na asubuhi moja, tulipanda kwenda huko mapema sana; tuliomba kwa ajili yake asubuhi ile ile, kama ilivyo kwenu, na hawawezi hata kuona alama yake. Anafanya kazi nyingi sasa kuliko alivyowahi kufanya. Yeye na maskini mke wake wamekuwa katika huduma ya Injili, labda kabla mimi sijazaliwa [Ndugu Kidd anasema, “miaka hamsini na mitano”—Mh.] Mnasikia hilo?—miaka hamsini na mitano. Kabla hata ya mimi kuja duniani walikuwa wakihubiri Injili. Na huyu hapa, ameponywa kwenye umri wa yapata miaka sabini na mitano—au themanini na mmoja. [Ndugu Kidd anazungumza tena na Ndugu Branham—Mh.] Ufufuo wa majuma mawili, ndiyo kwanza aendeshe ufufuo wa majuma mawili na akahubiri kila usiku. Umri wa miaka themanini na mmoja, ameponywa kansa.

Sawa, Dada, ni wakati wako sasa. Unaamini? *(Twendeni Askari)* Sawa, Dada, wewe, kwa kila mmoja wenu, tutafanya nini? BWANA ASEMA HIVI. Unafanya nini hapa, Shetani, umeshindwa. Tunakuja huko sasa. Tunaenda kwenye Nchi ya Ahadi. Ni kitu gani? Huu mlima wanaourundika mbele yetu ni kitu gani? Ni nani huyu asimamaye mbele pale, utakuwa tambarare? Vipi? Kwa Upanga wenye makali kuwili tutamkatakata kabisa. Hilo ni kweli. Vema.

Twendeni askari,
Watu wa Mungu;
Yesu yuko mbele.
Tumwandame juu;
Ametangulia (pamoja na Neno Lake)

Bwana vitani,
Twende mbele
Kwani Ndiye amani
Twendeni askari
Watu wa Mungu;
Yesu yuko mbele,
Tumwandame juu.

Haleluya! Walifanya nini? Kitu kilichotangulia vitani kwa ajili ya Israeli, kitu kilichotangulia kilikuwa ni nini? Waimbaji walitangulia kwanza. Nini kilichofuatia? Sanduku la Agano, halafu vita. Sawa! Unaamini sasa? Tutaimba, *Twendeni Askari;* tunaondosha kila shaka. Tukisimama kwa miguu yetu sasa, tunaenda vitani. Hebu na tusimame sasa, kila mmoja.

Twendeni askari,
Watu wa Mungu;
Yesu yuko mbele,
Tumwandame juu;
Ametangulia
Bwana vitani, (Tunamshindaje? Kwa Neno Lake)
Twende mbele
Kwani Ndiye amani.

Twendeni askari
Watu wa Mungu;
Yesu yuko mbele,
Tumwandame juu.

Hatutengwi nao,
Moja imani,
Tumaini moja,
Na mmoja upendo . . .

Wote ambao wanamwanimi Mungu waseme, "Amina!" [Kusanyiko linajibu, "Amina!"—Mh.] Haleluya! Mnaamini hilo? Sisi tu washindi. Yuko wapi kila adui? Chini ya miguu yetu. Sisi tu nini leo? Tumefufuka katika Kristo! Sasa, imekwisha, Dada. Unaamini jambo hilo? Unaweza kwenda nyumbani sasa. Unajisikia mzima? Anasema anajisikia mzima sasa, kila kitu ni shwari. Wangapi nje huko wanajisikia wazima?

Na walipopiga kelele, zile kuta zilianguka chini nao wakauteka (Amina!); waliuteka mji. Amina! Amina! Mnamwamini Yeye?

Sasa msisahau ibada ya usiku wa leo. Ndugu Neville atakuwepo hapa usiku wa leo akileta ujumbe wake, na Jumapili Jumapili inayofuata, Bwana akipenda, nitakuwa hapa. Sasa, hebu twendeni huku tukisogea mbele, na sasa, nje kutoka humu jengoni, hebu twendeni tukiimba *Twendeni, Askari,* na tangu leo na kuendelea, usiurudishe kamwe Upanga ule alani tena.

Uchomoe; hebu na tushinde. Wao walitoka wakishinda tena wapate kushinda. Sawa. Tena kwenye ubeti wa kwanza.

Twendeni askari,
Watu wa Mungu;
Yesu yuko mbele,
Tumwandame juu,
Ametangulia
Bwana vitani,
Twende mbele
Kwani ndiye amini.

Twendeni askari
Watu wa Mungu;
Yesu yuko mbele,
Tumwandame juu.

Vita Vikuu Sana Vilivyowahi Kupiganwa SWA62-0311
(The Greatest Battle Ever Fought)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi Machi 11, 1962, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1991 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org